**MAKALLA:** Una makandokando, huna chako uteuzi wa CCM

UKURASA 3

**HOJA** mpya kwa wabakaji, walawiti wafutiwe dhamana

UKURASA 4



UKURASA 11

**UNDANI** wa Samia, Hichilema kufufua TAZARA wakiwa kwa mwezeshaji wao China




ndani wa Samia, Hichilema 'kuifufua' AZARA kwa mwezeshaji wao China

eyale ya Nyerere, Kaunda na Mao
ndari Dar, shaba Zambia kupaishwa
na bandari kavu, umeme unapelekewa
shara mahindi sokoni Sh. bilioni 650

kainde Hichilema wa Zambia, Dk. Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wao, Rais Xi Jin-hina, walipokutana katika kikao cha faragha, kwenye Mkutano wa Ushirikiano Kati ya China wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

Orwa

ii inahesabika neema a mafanikio ya utawala Dk. Samia Suluhu, akiingi- npya ya maendeleo, pale hwa mradi mkubwa njia ya usafiri ya Mam- ya Tanzania na Zambia liokuwa unalega. wa wazo la ujenzi uli- ka 1968, ukaanza miaka daye, kisha huduma zi- nyika, 1976. na zao la ubunifu na

urafiki kati ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, swahiba wake kisiasa, kijamii na kiitikadi, jirani Rais Kenneth Kaunda wa Zambia na komredi wao, Mao Tse Tung wa China.

Serikali ya Mao Tse Tung, ilitoa mkopo usio na riba kwa mradi huo wa marafiki, wajenzi wakitoka China. Hivyo, kinachofanyika sasa katika Serikali ya Awamu ya Sita, ni mwendelezo wa maono yaliyoibuliwa na Nyerere, miaka saba baada ya uhuru, leo ikielekea mwaka wa 67 wa maadhimisho hayo.

Ni mtazamo uleule uliowasilishwa hivi karibuni katika safu hii, Serikali ya Awamu ya Sita, inavyoendeleza mashirika ya umma, kwa mwongozo wa Mwalimu Nyerere, ila mahitaji ya sasa.

Hadi sasa nchini kuna miradi mikubwa ya namna hiyo inayoendelezwa ya Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, ambalo ni wazo la Baba wa Taifa, aina yake ya fikra ikiendelezwa katika reli nchini.

Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) ulioasisiwa kwa maono ya Serikali ya Awamu ya Nne, wote wakiwa waumini wa itikadi ya serikali ya Nyerere na dira yake.

Wakati mradi wa reli ya TAZARA ilianza kutumika mwaka 1976, ulikuja na sifa iliyoko leo ya mradi unaondelezwa kwa jina la Reli ya Kisasa (SGR), ambayo upana wa reli unazidi ule mkongwe Reli ya Kati ya TRC.

Pia, ujenzi wa sakafu yake imetandikwa nguzo za zege na kokoto nyingi, tofauti na ile kongwe yenye nguzo chuma ambayo reli yake pia nyembamba kulinganisha na SGR inayotajwa imara na salama zaidi; Reli ya TRC ilijengwa mwaka 1905 na kazi ya upimaji ilianza 1894, katika Utawala wa Koloni la Kijerumani.

Wiki hii China, Tanzania na Zambia zimetia saini makubaliano ya awali kuifanyia matengenezo reli ya Tanzania hadi Zambia kukilenga kuboresha usafirishaji katika ukanda huo wenye utajiri wa rasilimali.

Wakati mkataba wa awali ulihusisha wazee; Mao Tse Tung, Nyerere na Kaunda, wa sasa ni marais wa Zambia, Hakainde Hichilema na Dk. Samia, na mwenyeji Rais Xi Jinping wa China, wote wakihudhuria Mkutano wa Ushirikiano Kati ya Afrika na China.

Mradi wa kwanza wa TAZARA, reli yenye urefu wa kilomita 1,860, ulijengwa kati ya mwaka 1970 na 1975 kwa mkopo usio na riba kutoka China, malengo ni kusafirisha mizigo kutoka migodi ya madini ya shaba na kobalti ya Zambia hadi bandarini, Dar es Salaam, Tanzania.

Ujenzi huo ulihusisha madaraja mengi, njia za chini na mapango, ikijumuisha wafanyakazi wa China zaidi ya 20,000 na wenyeji wa nchi hizo mbili.

Mradi wa TAZARA unaunganisha huduma ya abiria na mizigo kati ya bandari ya Dar es Salaam na kituo cha New Kapiri Mposhi, iliyopo kwenye njia ya reli kati ya Lusaka na Kitwe, ukanda wa shaba wa Zambia, ukichangia uhusiano wa kiuchumi na kibiashara kati ya nchi hizo.

Kisiasa, ililenga usafirishaji shaba ya Zambia wakikwepa bandari za Afrika Kusini iliyokuwa na serikali ya kibaguzi, pia Msumbiji, ilipokuwa koloni la Ureno.

China ikaunga mkono kwa kuwekeza katika uhusiano na msimamo huo wa mataifa huru ya Afrika, ikajitolea kudhamini mradi uliowezesha Zambia njia nyingine ya kufikia bahari.

Reli hiyo inatajwa ilipoanza kazi mwaka 1976, ilikuwa na vichwa 120 na mabehewa zaidi ya 2,000, sasa zinakadiriwa ni wastani wa vichwa 30 na mabehewa 100, huku hali ya reli na mtaji wa shirika si mzuri.

Ni njia inayopita kati ya misitu mapori, mapango makubwa na ya kuvutia nchini katika mikoa ya Kusini, Tanzania.

VITUO MUHIMU TAZARA
- Dar es Salaam
- Kidatu (kiungo na Shirika ya Reli Tanzania kwenda Kilosa na Dodoma)
- Ifakara
- Mlimba
- Makambako
- Mbeya

Inaendelea Uk 12


# Nipashe

Ijumaa Septemba 6, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581791

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII


www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

## WATAFITI MUHIMBILI

# Dawa za VVU zajenga usugu



UKURASA 3




Maduka na magari yakiwa yamezingirwa na maji ya mafuriko kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge maarufu ITV, Dar es Salaam, baada ya mvua kunyesha jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Vijiji vinne na faini za mbuzi, ng'ombe; asiyelipa hazikwi

UKURASA 2

## CHADEMA sasa yahamia katika maombezi ya kuing'oa CCM

UKURASA 2

**MICHEZO** FADLU ALETA MFUMO MPYA SIMBA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Rufaa Jacobs Mwambegele (kulia), akiongoza kikao cha tume cha kawaida kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaoendelea nchini, Mjini Unguja Zanzibar jana. **PICHA: INEC**

# Vijiji vinne na faini za mbuzi, ng'ombe; asiyelipa hazikwi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

TAHARUKI imezuka katika vijiji vinne vilivyoko Kata ya Kisiriri, wilayani Iramba, mkoani Singida, baada ya kuibuka vikundi vya kimila, maarufu Nkiri, vinavyodaiwa kutoza faini ya ng'ombe, mbuzi au fedha, na asiyetoa hutengwa katika shughuli za kijamii.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini vikundi hivyo vina safu za viongozi wake na mwananchi asiyetoa faini hiyo, hutengwa na kijiji au kitongoji na haruhusiwi kwenda dukani kununua bidhaa yoyote.

Kadhalika, haruhusiwi kwenda kusaga nafaka wala kwenda katika huduma za afya kupata matibabu na hawaruhusiwi kuhudhuria msiba utakapotokea katika eneo anamoishi na atakapofiwa hakuna atakayemfariji na atakayeonekana kafanya hivyo naye anatozwa faini.

Imebainika pia kuwa vikundi hivyo ambavyo vipo kila kijiji na kila kitongoji, vina sheria zao walizojiwekea, viongozi wa maeneo husika wakidaiwa ni sehemu ya wanufaika wa fedha zinazotozwa, hivyo kushindwa kuchukua hatua.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hii kwa takribani miezi miwili, umebaini tatizo hilo ambalo limegeuka kero kubwa kwa wananchi ambao kila wanapolalamika, hakuna hatua zinazochukuliwa.

Uchunguzi umebaini wananchi wanaokubali kutoa ng'ombe au mbuzi, mifugo hiyo huchinjwa na nyama kugawanywa kwa watu wote wa kijiji au kitongoji husika.

Mmoja wa wananchi waliokumbwa na kadhia hiyo ni Mzee Wilfred Tuntuma, ambaye alisema ametozwa faini ya ng'ombe watatu baada ya kutuhumiwa kuhusika na tukio la mauaji ya Daudi Kitonka lililotokea Agosti 30, 2023.

Tuntuma alisema kuwa baada ya tukio hilo la mauaji kutokea katika Kijiji cha Kinalilya, walikamatwa watuhumiwa 10, akiwamo yeye, lakini Mei 13, 2024, Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma ilimwachia huru baada ya kubaini hakuhusika na mauaji hayo.

Alisema kuwa baada ya kurejea kijijini kwake, viongozi wa kikundi cha Nkiri, walimtaka alipe faini ya ng'ombe hao, lakini amekataa kutoa kwa sababu mahakama imebaini hakuhusika na mauaji hayo.

Tuntuma alisema viongozi wa kikundi hicho licha ya kuwapatia nakala ya hukumu ya mahakama inayoonesha kutohusika kwake katika mauaji hayo na nakala nyingine kuzipeleka kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kinalilya na kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kisiriri, wameshikilia msimamo wa kumtaka alipe faini hiyo.

Mzee huyo alisema kuwa baada ya kushikilia msimamo wa kukataa kutoa faini hiyo, ametengwa na jamii na haruhusiwi kwenda kununua mahitaji yoyote katika maduka matatu yaliyoko Kitongoji cha Shigani ambako anaishi.

Kadhalika, alisema amekatazwa na jamii kwenda kusaga katika mashine iliyoko katika kitongoji hicho na hivi karibuni kulipotokea msiba wa Nakembekwa Mathayo, alipohudhuria alifukuzwa na viongozi wa kitongoji.

Tuntuma alisema kuwa kutokana na kutengwa na jamii, hivi sasa anaishi kama yuko kisiwani na maisha yake yako hatarini, "kwa kuwa imefika wakati wananitishia maisha".

Kutokana na hali hiyo, Mzee Tuntuma ameomba serikali ngazi ya wilaya kuingilia kati suala hilo.

Alisema wenzake tisa aliokamatwa nao katika kesi ya mauaji, ndugu zao walibanwa na kikundi hicho na walitoa faini ya ng'ombe mmoja wakiwa gerezani na kuchinjwa na nyama kugawiwa kijijini.

### KAULI YA MTENDAJI

Mtendaji wa Kata ya Kisiriri, Sihaba Mohamed, alikiri kutambua vikundi hivyo vilivyoko katika vijiji vya kata hiyo ambavyo ni Kisiriri, Kisimba, Kisana na Kinalilya vinavyotoza faini wananchi.

Alisema vikundi hivyo vya kimila vina sheria zao ambazo zinatekelezwa katika kila kijiji na kitongoji ambapo mtu akifanya tukio lolote tofauti na taratibu zao, huitwa na kupigwa faini ya ng'ombe, mbuzi au fedha.

"Ukifanya kosa halafu ukapigwa faini, mfano wanasema 'tunataka ng'ombe watatu au mbuzi mmoja', ukigoma kulipa, wanasema 'wamekusamehe', lakini baada ya hapo hutaruhusiwa kusaga nafaka katika mashine. "Kama kuna duka hutaruhusiwa kununua vitu, ukifiwa hawajui na hata kupewa lifti katika pikipiki hutaruhusiwa.

"Suala hili ni changamoto, labda kama inawezekana viongozi wa ngazi ya mkoa waingilie kati ili vikundi hivyo vivunjwe.

"Hii wilaya (Iramba) ina kata 20 na katika kila kata Nkiri ipo, labda tukae katika Kamati ya Ulinzi na Usalama tuongee suala hili. Katika kata yangu kuna vijiji vinne na vyote vina vikundi hivyo," alisema Mohamed.

Kuhusu madai ya Mzee Ntutuma, Mtendaji huyo alisema kuwa Septemba 3, 2024 aliwaita viongozi wa kikundi anakotoka mzee huyo kuongea nao na kukubaliana apunguziwe adhabu badala ya ng'ombe watatu, atoe mmoja.

Ni faini inayopendekezwa dhidi ya mzee huyo ilhali Mahakama Kuu ilishasema hana hatia ya mauaji.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alipotafutwa na Nipashe jana, alisema serikali inaendelea kufuatilia mambo hayo ambayo alisisitiza yako kinyume cha sheria za nchi.

# CHADEMA yahamia katika maombezi kuing'oa CCM

**Na Steven William,** MUHEZA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimegeukia katika maombi, kikiwataka Watanzania kumwomba Mungu ili katika uchaguzi ujao, Chama Cha Mapinduzi (CCM) king'oke madarakani.

Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika aliyasema hayo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Majengo Shimoni, wilayani Muheza, mkoani Tanga.

Alisema wananchi wanapaswa kufanya hivyo kwa kile alichodai CCM inawapa shida wananchi katika nchi yenye utajiri.

Mnyika alisema Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa, lakini wanaofaidika ni viongozi huku wananchi wakibaki maskini.

Katibu Mkuu huyo pia alionya watendaji wa serikali kuacha mara moja tabia aliyodai "kuibeba CCM katika uchaguzi", akisisitiza CHADEMA wako macho kuhusu hilo.

Katika hilo la madai ya watendaji wa serikali kuibeba CCM, akiwa mkoani Arusha jana, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla alisisitiza chama hicho kinashinda kwa haki na kitaendelea kushinda kwa haki kutokana na mikakati yake, ukiwamo utekelezaji ilani ya uchaguzi.

Katibu Mkuu Mnyika pia aliwataja viongozi na wanachama wa CHADEMA kujipanga ipasavyo kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuongoza vijiji, vitongoji na mitaa nchini.

"Viongozi wa CHADEMA na wanachama mnapaswa kujiandaa ili kushiriki na kushinda nafasi za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa ili kuibwaga CCM," alisema.

Mnyika alisema ushindi wa nafasi hizo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakuwa mwanga na dira ya ushindi wa Uchaguzi Mkuu mwakani katika nafasi ya urais, ubunge na udiwani.

Aliwataka wananchi kuacha kile alichokiita "uteja wa CCM" badala yake wakikatae kuanzia uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa kwa kuichagua CHADEMA.

Alisema serikali imeleta ugumu wa maisha kwa kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi hasa kwa bidhaa muhimu ikiwamo sukari.

Mbunge mstaafu wa Viti Maalum CHADEMA, mkoani Tanga, Yosepha Komba, alidai kuna baadhi ya viongozi wa CCM wanatuma vijana wao kuharibu bendera za CHADEMA nyakati za usiku.

**HABARI KITAIFA**



Mbunge mpya wa Bunge la Afrika Mashariki, Dk. Gladness Salema, akiwashukuru wabunge baada ya kuchaguliwa kwa kura 254, bungeni, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

### WATAFITI MUHIMBILI

# Dawa za VVU zajenga usugu

**Na Grace Mwakalinga**

UTAFITI uliofanywa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), umeonesha asilimia 5.8 ya Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) na kutumia dawa, wanakabiliwa na tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo.

Mtafiti Mwandamizi Kitengo cha Maikrobaiolojia na Kinga MUHAS, Dk. Doreen Kamori, aliyabainisha hayo juzi wakati wa Kongamano la 11 la chuo hicho lililoandaliwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya usugu wa vimelea dhidi ya dawa za kupunguza makali ya VVU na mapendekezo kukabiliana na tatizo hilo.

Dk. Doreen alisema walifanya utafiti huo mwaka 2020 katika mikoa 22 Tanzania Bara, ikiwamo Songwe, Mbeya, Iringa na Njombe.

Alitaja sababu zinazochangia tatizo hilo ni pamoja na kuingizwa nchini dawa ambazo zinachangia usugu na watu kutokuwa wafuasi wazuri wa kutumia dawa.

Alitoa ushauri kwa serikali wanapofikiria kubadilisha dawa au kuingiza nchini ni vyema kuweka miongozo na kufanya utafiti kufahamu wingi wa VVU kwa wagonjwa na kuangalia namna ya kuboresha.

"Ni vyema kuweka miongozo na kujiandaa vizuri kumudu tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa za kupunguza makali ya VVU au kudhibiti kabla ya dawa hizo kuleta madhara," alisema Dk. Kamori.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Said Aboud, alisema kongamano hilo limetoa nafasi ya kubadilishana uzoefu na kukubaliana namna sahihi ya kukabiliana na tatizo hilo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa za kupambana na VVU.

Alisema tatizo hilo linazidi kuongezeka kwa sababu WAVIU wanaendelea kutumia dawa maisha yao yote, hivyo ni muhimu kuweka mikakati, ikiwamo kufuata maelekezo ya daktari na mwongozo unaotakiwa wakati wa kutumia dawa hizo.

Mtu anayeishi na VVU, anapaswa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu kutoka kwa daktari badala ya kutumia dawa kiholela. Hii itasaidia kukabiliana na tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa (UVIDA).

"NIMR inatekeleza Mpango wa Taifa Kudhibiti Kupambana na Magonjwa ya Kuambukiza, yakiwamo maambukizi ya VVU na UKIMWI, tunatekeleza afua mbalimbali katika mapambano hayo ili kuwasaidia kuboresha maisha yao na kuchangia nguvu kazi ya taifa," alisema Prof. Said.

Kaimu Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Emmanuel Balandya, alisema asilimia 4.5 ya watu wazima nchini sawa na watu 1,548,000 nchini, wanaishi na VVU. Kati ya hao, wanaotumia dawa, asilimia tano tayari wana usugu wa vimelea dhidi ya dawa (UVIDA).

Naibu Makamu Mkuu wa MUHAS Idara ya Fedha, Mipango na Utawala, Prof. Erasto Mbugi, alisema wanafanya makongamano kama hayo ili kufanya tathmini ya gharama mtu au jamii anayoipata kutokana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

Alisema kuwa bila kuweka mikakati ya kupambana na tatizo hilo, wananchi wataendelea kutumia gharama kubwa kutibu usugu wa vimelea hivyo dhidi ya dawa.

# 'Afande' atinga mahakamani

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma imeahirisha shauri lililofunguliwa na Wakili Paul Kisabo dhidi ya Fatma Kigondo anayetuhumiwa kutuma vijana kumbaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam.

Kesi hiyo imeahirishwa kutokana na hakimu aliyekuwa anasikiliza shauri hilo kuhamishwa kituo cha kazi huku shauri hilo likiwa halijapangiwa hakimu mwingine.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa jana katika mahakama hiyo.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo baada ya kuahirishwa kwa shauri hilo, Wakili Paul Kisabo alidai sababu za kuahirishwa ni kuhamishwa kituo cha kazi kwa hakimu aliyepangiwa kesi hiyo. Imepangwa kutajwa Oktoba 7, mwaka huu.

"Leo (jana) kama mlivyoona, mshtakiwa tayari amefika mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma na kusomewa mashtaka yanayomkabili," alidai wakili huyo.

Kesi nyingine namba 23476 ya mwaka 2024 ya ubakaji kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile, imeendelea kusikilizwa katika mahakama hiyo kwa upande wa Jamhuri kuendelea kutoa ushahidi wao.

Washtakiwa katika kesi hiyo ya jinai ni askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) MT 140105 Clinton Damas, maarufu Nyundo, Askari Magereza C.1693 Praygod Mushi, Nickson Jackson 'Machuche' na Amin Lema 'Kindamba'.

Wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti huyo wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam. Kama wakipatikana na hatia, watakumbana na adhabu ya kifungo cha maisha kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

# Makalla: Kama una makandokando, huna chako kwenye uteuzi wa CCM

**Na Salome Kitomari,**
LONGIDO

KATIBU wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesisitiza chama hicho hakitaki mgombea mwenye 'makandokando' ambaye lazima watumie sabuni na dodoki kumsafisha, bali kinataka anayekubalika kwa wananchi.

Amesema chama hicho kamwe hakishindi kwa hila bali kwa haki na kwamba hakihitaji kubebwa, bali utekelezaji ilani yake ni kielelezo kizuri kwa wananchi.

Makalla aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa CCM kuanzia ngazi ya shina hadi mkoa kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema CCM inahitaji wapigakura milioni 12 kushinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Novemba mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Makalla aliwataka wana CCM kuendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura ili kuwa na sifa ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa.

"Ninawahakikishia kuwa CCM itateua wagombea safi wasio na makandokando. Ninawaagiza viongozi wa chama kuzingatia hili ili kupata wagombea wanaowajibika kwa wananchi.

"Wasiosoma taarifa za mapato na matumizi ya vijiji, uchaguzi ujao hawana nafasi. Jitahidini mchague wenyeviti ambao hawana makandokando, hatutaki mgombea ambaye tumwoshe kwa dodoki na sabuni.

"Tunataka mtu ambaye tukimpeleka kwa wananchi wanamkubali na hakuna minong'ono. Chagueni watu sahihi ambao watatoa matumaini kwa CCM. Chama kinataka uchaguzi wa kishindo na heshima.

"Tusiudharau, tusibweteke, tuweke malengo na mikakati tushinde kwa kishindo. Upo umuhimu na sababu za kushawishi marafiki zetu, wapenda maendeleo watunze imani," alisema Makalla.

Alisema umuhimu wake ni katika mafanikio yote waliyonayo ya utekelezaji ilani kwa amani na utulivu kuanzia wenyeviti wa kitongozi, mitaa, vijiji, madiwani, wabunge na Rais.

Makalla alisema iwapo watakuwa na kiongozi wa upinzani, kuna siku watapeleka maombi ya kujenga madarasa, lakini akasema hakuna eneo la kujenga.

Alijinadi kuwa akiwa wa CCM ataongea na wenzake wa CCM na kutekeleza mradi, ndio maana ni muhimu kuhakikisha wanakiweka chama hicho madarakani.

Kuhusu changamoto zilizoko katika jamii za wafugaji, Makalla alisema serikali inaendelea kuzitatua na mafanikio waliyoyapata ni kutokana na utekelezaji ilani.

"Uhai wa chama chetu ni kuimarisha mabalozi, CCM ina mtaji wa mabalozi, muundo wa CCM ni muundo wa chama imara. CCM inatajwa ni chama namba moja Afrika na namba tisa duniani, sifa hizi ni kutokana na kazi nzuri za mabalozi.

"Ninasimama kifua mbele kuwa msemaji wenu machachari, jeuri yangu ni mabalozi, ndio jeshi kubwa la CCM na jumuiya zake za wanawake, vijana na wazazi," alisema.

Makalla pia aliomba wana Longido kudumisha amani na umoja kwa kuwa ndio nchi ya mfano yenye makabila mengi 120, lakini hakuna kubaguana.

Alisema walikabidhiwa nchi wakiwa wamoja na hakuna Tanzania nyingine na kila Rais anaahidi kulinda umoja na mshikamano wa nchi.

"Rais Samia anawapenda Watanzania wote, amethibitisha hilo kupitia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

"Kuna vyama vinataka kutugawa, vinataka faida ya kisiasa kwa kuonesha kabila fulani linabaguliwa, jambo ambalo si kweli.

"Rais Samia anataka umoja na mshikamano wa kujenga Tanzania. Ogopa sana mtu mfitini, msikubali kufitinishwa, wapo wanasiasa wafitini wangependa tusiwe wamoja," alisema Makalla.

Akiwa katika Kituo cha Pamoja cha Forodha cha Namanga, mkoani Arusha, Makalla alitaka taasisi zote kuongeza kasi ya kuhudumia malori ya mizigo yanayokwenda nchi jirani ya Kenya na kuharakisha biashara baina ya pande zote.

Alisema amefurahishwa na mikakati ya kituo hicho upande wa Tanzania, kuhakikisha malori yanapita katika ukaguzi kwa haraka na kuendelea na safari.

Katibu Mkuu huyo alisema Rais Samia na Rais wa Kenya, William Ruto, wanashirikiana kuhakikisha biashara eneo la mpaka inakuwa rahisi kwa manufaa ya wananchi wote.

"Tuongeze kasi ya kuwezesha mizigo kupita, tuondoe kero ya foleni ya malori, wasikae muda mrefu wanaposubiri ukaguzi, ili kuhakikisha biashara inakwenda kwa wakati," aliagiza.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Salum Kali, alisema atasimamia kwa karibu kwa kuondoa kero zote katika mpaka huo ili kuhakikisha biashara inafanyika bila tatizo.

## Waziri ahimiza madaktari moyo wa huruma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka madaktari kuendelea kuwa na moyo wa huruma na upendo katika kuwahudumia wagonjwa.

Amesema madaktari hao wanapaswa kutambua kuwa Mungu anawatumia katika kuponya magonjwa.

Simbachawene alitoa rai hiyo juzi alipofungua Mkutano Mkuu wa 87 wa Mwaka wa Chama cha Madaktari Wakikristo Tanzania (TCMA) katika Ukumbi wa Mikutano wa St. Gaspar, Dodoma.

"Nimefurahi kusikia kwamba chama chenu kinatimiza miaka 87 tangu kianzishwe na kina wanachama takribani 300 na hamjawahi kushindwa kukutana hata mara moja, hivyo mnapata fursa ya kujadili mambo muhimu kuhusu huduma za afya na ustawi wa jamii," alisema.

Waziri alisema anafahamu kuwa katika msingi na Sera za makanisa ya Kikiristo kuna utaratibu wa kuwasaidia wasiojiweza, hivyo aliomba taasisi hizo kuendelea na utaratibu huo kwa kuwa serikali iko pamoja nao wakati wote kwa manufaa ya umma.

Pia alizishauri taasisi hizo za Kikiristo kutazama upya namna bora ya usimamizi hospitali na vituo vyao vya afya kwa kuwa sehemu nyingi kumekuwa na tatizo la kushindwa kuviendesha kutokana na watumishi wao kutokuwa weledi katika kazi, kushindwa kwenda sambamba na mahitaji ya wateja na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Awali, Rais TCMA, Gresmus Ssebuyoya, alisema wanachama hao hukutana kila mwaka kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujifunza na kuainisha changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa shughuli, kuziweka pamoja na kuziwasilisha kwa maaskofu kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi.

"Chama kiko tayari na kitaendelea kushirikiana na serikali katika kutoa huduma za afya kwa wananchi na kuboresha huduma za afya kwa watu wenye uwezo mdogo wa kumudu gharama za afya," alisema.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni, "The Future of Healthcare: Innovation and Solution for future" ikilenga kuwasaidia madaktari katika kujiandaa na kutekeleza mkakati wa utoaji wa huduma ya afya kwa wote na kukabiliana na mazingira ya utoaji wa huduma za afya ambayo yanabadilika haraka na kuongezeka kwa malalamiko ya kukosekana kwa maadili kwa watumishi wa afya nchini.



Msaidizi wa Kisheria na Mratibu wa Shirika la Liwale Women Paralegal Aid and Unity (LIWOPAU), Hidaya Chikawe (kulia), akikabidhi kipeperushi chenye ujumbe unaohusu uboreshaji wa daftari la wapigakura, kwa Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima cha Hiari Moyo, Ramadhan Mpimbita, wakati shirika hilo lilipokwenda kuhamasisha wananchi kujiandikisha na kuboresha taarifa zao, katika Kata ya Mpigamiti, mjini Liwale mkoani Lindi, juzi. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpigamiti, Sadick Tewele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoja mpya kwa wabakaji na walawiti wafutiwe dhamana

**Na Halfani Chusi**

WATETEZI wa haki za binadamu wameshauri serikali iondoe dhamana katika makosa ya ubakaji na ulawiti ili kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyoendelea kujitokeza ndani ya jamii.

Ushauri huo umetolewa baada ya hivi karibuni kuripotiwa tukio la baba kudaiwa kunajisi mwanawe wa miezi sita, ukatili uliosababisha kifo cha mtoto huyo.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam kwa niaba ya wanaume, Bushiri Khalfani, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua kali kwa wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Alisema mbali na kuchukua hatua kali zaidi pia, atoe tamko kama alivyofanya kwa watekaji siku chache zilizopita.

"Sisi wanaume masuala haya yanaleta fedheha na aibu kwa taifa letu, mtu akituhumiwa dhamana asipewe, ikiwezekana akatwe uume, anyongwe hadharani, iwe fundisho kwa wanaume wanaofanya vitendo hivi.

"Sisi kama wanaume tunajisikia aibu wenzetu wanavyofanya vitendo hivyo, wapo wengine wanadanganywa na waganga wa jadi kwamba watapata utajiri.

"Tunaomba kupitia vyombo vya habari serikali isikie na kuchukua hatua kali dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kunyimwa dhamana," alisema.

Maumba Likado kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa Kitunda, jijini Dar es Salaam, alisema kuwa zamani baba alikuwa rafiki wa mtoto, lakini hivi sasa amekuwa adui.

Alisema vitendo hivyo havipendezi na vinatia aibu katika jamii na kupendekeza kwamba kesi za namna hiyo zinapofikishwa mahakamani zisichukue muda mrefu.

Erasto Basili alisema, "Tunaona namna serikali inavyoshindwa kutilia mkazo matukio haya, ndio maana kila siku yanajirudia, halafu mtu anawekewa dhamana anatoka kesho unamwona mtaani. Hii inauma sana.

"Ikiwezekana mtu akikutwa na hatia hiyo anyongwe kwa sababu mtu anayeweza kumlawiti mtoto wake, hawezi kumwogopa mtu mwingine," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Zainabu Mmari, alisema anatamani hatua kali za kisheria kwa aliyehusika na ubakaji kwa mtoto huyo na haki itendeke.

"Tumeona tukio hilo (baba kunajisi mwanaye) limeathiri jamii, serikali ichukue hatua za makusudi na mama wa mtoto huyo apate msaada wa kisaikolojia ili akae sawa.

"Hili si suala dogo, matukio mengi yanaripotiwa, tuombe jamii na kila mtu achukue hatua, ili mwisho wa siku tutokomeze ukatili wa kijinsia kwa pamoja," alisema Zainabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema kila mtu ana haki ya kuishi katika mazingira salama na kusisitiza, kitendo cha baba kumnajisi mtoto wake wa miezi sita ni aibu kwa taifa.

"Kwa kweli hatua za haraka zinatakiwa zichukuliwe kwa watu wanaofanya vitendo hivi havipendezi vinatia uchungu.

"Ninajifikiria ninajiweka katika nafasi ya yule mama wa mtoto sijui anajisikiaje sasa hivi athari aliyopata haitasahaulika. Mamlaka za juu kabisa ziingilie kati suala hilo.

"Serikali, Jeshi la Polisi wanatakiwa waione hii kama dharura, nilitarajia hata bungeni kwa tukio la mtoto huyu kungekuwa na mjadala wa dharura kwa sababu hii sasa imezidi," alisema Lilian.

Alisema anahitaji kuona wanaokutwa na hatia ya kutenda vitendo hivyo, wanafungwa kifungo cha maisha na si miaka 30, ili liwe funzo kwa wengine.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi wa Fursa Pamoja na Harakati wa TGNP, Flora Ndaba, alisema inatia uchungu kwa mama aliyetoka leba na kuvuka kiunzi cha kifo, leo analia kwa kuona mtoto wake amekufa kwa kubakwa na baba yake mzazi.

"Imefika hatua sasa wanaume wakutane waulizane, waongee jambo hili likomeshwe, ifike hatua haya masuala yawe historia. Huyu mama asaidiwe lakini pia tukumbuke haya matukio ya aina hii yamejitokeza mengi," alisema Flora.

# Dirisha kushindania tuzo za uandishi bunifu lafunguliwa

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa Kamati ya Taifa ya Tuzo za Uandishi Bunifu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Penina Mlama, amesema dirisha la kuwasilisha miswada kwa ajili ya kushindania tuzo hiyo limefunguliwa rasmi na maandiko yatapokelewa kupokelewa hadi Novemba 30, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Prof. Penina alisema ni awamu ya tatu ya utoaji tuzo hizo ambazo zilianzishwa 2022 chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na inaratibiwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

Alisema tuzo hiyo ilipoanzishwa ilihusisha nyanja mbili za uandishi bunifu ambazo ni riwaya na ushairi, na kwamba kwa sasa imeongezeka ya hadithi za watoto, pamoja na tamthiliya za jukwaani, redio na runinga.

"Kuna vigezo vinajumuisha nyanja zote nne ambavyo wanaowasilisha miswada wanapaswa kuvifuata, ikiwamo kila mshiriki awe raia wa Tanzania, andiko bunifu liwe katika lugha ya Kiswahili, mwandishi anaruhusiwa kushiriki andiko moja katika nyanja atakayoichagua.

"Vingine ni sehemu yoyote ya mswada isiwe imechapishwa eneo lolote ikiwamo kuonyeshwa jukwaani, wakati wa kuwasilisha mwandishi atatakiwa kutia saini tamko maalumu kuthibitisha kuwa kazi anayoiwasilisha ni ya kwake na haijawahi kuchapishwa mahali kokote," alisema Prof. Penina.

Aidha, aliongeza kuwa kigezo kingine ni waandishi walioshinda nafasi ya kwanza hadi tatu katika tuzo hiyo kwa miaka iliyopita hawaruhusiwi kushiriki kwenye nyanja yoyote ile kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka alioshinda, pia mswada ulioshika nafasi ya nne hadi 10 haitaruhusiwa kushiriki, lakini mwandishi anaweza kushiriki kwa kuwasilisha mwingine.

Vigezo vingine mswada utakaofaulishiwa kwenye tuzo nyingine hautazingatiwa, andiko bunifu litakalowasilishwa liwe makini lililojikita kwenye masuala muhimu ya kijamii, na mswada uwasilishe wazo asili la mwandishi.

Aidha, alieleza kuwa kuna vigezo mahususi kwa kila nyanja na kwamba kwa upande wa tamthilia mswada utumie vionjo vya sanaa za maonyesho vya kitanzania, ya jukwaani iwe ya dakika 40 hadi 60, pia iwe na maonesho yasiyozidi sita na wahusika sita.

Pia, alisema tamthilia ya luninga iwe na episodi 13, kila moja iwe ya muda usiozidi dakika 30, na ya redio iwe na vipade 13 vyenye dakika 30 na wahusika wasizidi saba.

Alisema kwenye ushairi, mashairi yasipungue 50 na yasizidi 60, idadi ya beti kwenye kila shairi isizidi 15, akieleza kuwa ikiwa muswada ni utenzi, basi uwe mmoja na wenye beti kati ya 300 na 400.

Vilevile, katika riwaya alisema urefu wake uwe kati ya maneno 60 na 100,000 na katika hadithi za watoto iwe na maneno kati ya 250 na 100,000, itakayowasilishwa ilenge watoto wa miaka mitano na 12, ijumuishe michoro, na iwe kwenye lugha inayoeleweka.

"Mshindi wa kwanza kwenye tuzo hizo atapata Sh. milioni 10, na mswada wake utachapishwa na serikali na kusambazwa mashuleni, pia anapata ngao na cheti, wa pili atapata Sh. milioni saba na cheti, na wa tatu Sh. milioni tano na cheti," alisema Prof. Penina.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (katikati), akizungumza katika kikao cha uwasilishaji wa taarifa ya mafanikio ya wilaya hiyo, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Dar es Salaam juzi. Kulia ni Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya hiyo, Shaweji Mkumbula. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CCM yamkana aliyekuwa DC Longido

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KATIBU wa NEC-Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesema chama hicho hakihusiki na maneno yaliyotolewa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi.

Amesema CCM inashinda uchaguzi kwa haki na si kubebwabebwa na itaendelea kushindana kutokana na namna ilivyojipanga vizuri.

Makalla aliyasema hayo jana mkoani Arusha wakati akizungumza na viongozi wa chama hicho baada ya kuwasili mkoani hapa na kupokewa kuanza ziara yake ya siku sita kukagua utekelezaji wa ilani ya chama.

Wiki iliyopita kulisambazwa video katika mitandaoni ya kijamii, ikimwonesha kiongozi huyo akiwaeleza madiwani wa Wilaya ya Longido kwamba hakuna aliyeshinda kwa nguvu zake, bali serikali iliwasaidia.

"Hata yule jamaa (akimlenga aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Longido) aliyoyasema si maneno ya chama, mimi kama Msemaji wa Chama, niseme yalikuwa maneno yake na ukimsikiliza alikosa hoja huko vichwani, sijui alifuata nini, sisi CCM hatujamtuma na hatuhusiki na maneno.

"Sisi tunajipanga kushinda kwa haki na imekuwa kawaida ya kushinda kwa haki, hivyo niwaambie wananchi, yalikuwa maneno yake na si msimamo wa chama," alisema.

Kuhusu mgogoro unaoendelea katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), alisema: "Sisi ni chama kiongozi tumekubali kutokwenda Ngorongoro, wenzetu waige mfano wetu.

"Nimekuja Arusha kwa ajili ya kumalizia maeneo ambavyo wakati tunakuja kwenye ziara ya Katibu Mkuu hatukufika Ngorongoro, Karatu na Monduli, lakini niliomba nafasi kwenda Ngorongoro kuzungumza na wananchi.

> **Na bila kuwa na msingi ndani ya serikali za mitaa, hata huko juu tukaja tukapata viongozi wazuri, bado watashindwa kufanya kazi, kwa sababu utakuwa msingi...**

"Tulivyoomba kibali, tulikatazwa na kwa sababu sisi ni chama kiongozi, tumekubali na wenzetu wajifunze kwetu na huu ni ujumbe kuwa tunaheshimu utawala wa kisheria," alisema Makalla.

Kauli ya mkuu wa wilaya ilizua mjadala mkali, ikitajwa inakwenda kinyume cha falsafa ya 4R ya Rais Samia Suluhu Hassan ambayo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya.

Baada ya video hiyo kusambazwa mitandaoni, Septemba Mosi mwaka huu, Rais Samia alitengua uteuzi wake katika nafasi hiyo aliyoitumikia kwa mwaka mmoja na miezi minane katika wilaya hiyo ingawa taarifa ya Ikulu haikuhusisha utenguzi huo na kauli yake inayonyooshewa kidole na CCM.

Juzi mchana Makalla aliwasili mkoani Arusha kuanza ziara yake ya siku sita katika mikoa ya Arusha na Manyara.

Kiongozi huyo alipokewa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Loy Sabaya pamoja na viongozi wengine wa chama mkoani hapa.

Makalla akiwa mkoani Arusha katika wilaya za Longido, Monduli na Karatu, atazungumza na wananchi kwenye mikutano ya nje na kwamba na mikutano ya ndani yote inalenga kukagua uhai wa chama pamoja na kusikiliza kero za wananchi kisha kuzipatia majibu. Baada ya kukamilisha ziara mkoani Arusha, atakwenda Manyara katika wilaya za Babati na Simanjiro ambako pia atakuwa na mikutano ya ndani na nje kwa ajili ya kusikiliza wananchi na kufuatilia utekelezaji Ilani ya CCM.

# Benki Maendeleo kuchangia ujenzi kituo watoto wenye matatizo ya akili

**Na Halfani Chusi**

BENKI ya Maendeleo inatarajia kuandaa mbio za marathon zenye lengo la kuhamasisha watu kuchangia vitanda katika Hospitali ya Kanda ya KCMC ya Mkoa wa Kilimanjaro na ujenzi wa kituo kipya cha kulea watoto wanaozaliwa na matatizo ya akili.

Mkuu wa Idara Biashara na Masoko wa benki hiyo, Emmanuel Mwaya, alisema katika mazungumzo na Nipashe kuhusu lengo la mbio hizo.

Alisema mara ya kwanza mbio hizo zilizofanyika mwaka jana na kuhudhuriwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye anatarajiwa kuhudhuria tena siku ya Jumamosi walifanikiwa kuchangisha Sh. milioni 120 ambazo zilisaidia kununua vitanda katika hospitali hiyo na nyingine zitasaidia katika ujenzi wa kituo hicho.

"Katika fedha hizo tulitoa Sh. milioni 60 tukanunua vitanda 12 tukapeleka katika hospitali ya KCMC kwa ajili ya kuwasaidia joto watoto wanaozaliwa kabla ya muda.

"Asilimia 25 ya watoto waliokuwa wanazaliwa katika hospitali hiyo, walikuwa wanakufa kwa kukosa joto, baada ya kupeleka msaada huo, vifo vimepungua mpaka kufikia asilimia 20, hivyo tukasema tunafanya tena mbio kwa ajili ya kusaidia tena hiyo hospitali na ujenzi wa hicho kituo ili kukidhi mahitaji yaliyosalia," alisema.

Alisema katika mbio za mwaka huu lengo lao ni kukusanya zaidi ya Sh. milioni 200 ambazo zitasaidia katika maeneo hayo.

"Mwaka jana lengo lilikuwa kukarabati hicho kituo, lakini isivyo bahati kilivamiwa na mafuriko ikashindikana, cha kushukuru watoto walikuwa likizo kwa hiyo kinajengwa upya katika Kijiji cha Kitopeni Bagamoyo ambako baada ya kuchangisha Jumamosi zitachanganywa na zile za mwaka jana kwa ajili ya kusaidia ujenzi wake," alisema Mwaya.

Mbio hizo zitafanyika kuanzia Oysterbay kutokea maeneo ya Viwanja vya Farasi zitahusisha umbali wa kuanzia kilomita 2.5, 5, 10 na 21 kupitia maeneo ya Daraja la Tanzanite, round about ya Aga Khan na Coco Beach.

Mwaya aliomba wadau kujitokeza siku hiyo kushiriki mbio hizo na kuchangia fedha kwa ajili ya kuokoa maisha ya watoto.

# Wakulima walalamikia wafugaji kulisha mifugo katika mashamba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa kabla ya mwaka 2024/25 kufika ukomo, serikali itakuwa imetoa mwongozo wa vijana kujitolea katika utumishi wa umma utakaozingatia masuala mbalimbali, ikiwamo namna ya kupata na kuwalipa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu aliyasema hayo jana wakati akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti maalum, Grace Tendega.

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kuhakikisha kunakuwa na utaratibu maalum wa kupata vijana wanaojitolea katika taasisi mbalimbali serikalini.

"Lini serikali itatoa mwongozo huo uliowekwa ili vijana wapate ajira kupitia utaratibu huo?" alisema.

Naibu Waziri Sangu, akijibu swali hilo, alisema serikali ipo mbioni kukamilisha mwongozo huo, hivi sasa inaandaa randama ambayo baada ya kukamilika utatolewa waraka wa namna ya kuwapata vijana hao.

Alisema utawekwa utaratibu wa ushindani ili kijana anayetaka kujitolea afanyiwe usaili.

"Kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha tutakuwa tumetoa waraka huu wa kuwaongoza wakuu wa taasisi namna ya kuwapata vijana wa kujitolea," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alitaka kujua kama serikali iko tayari kuwalipa posho ya kujikimu wafanyakazi wanaojitolea ili kuondoa matabaka ya malipo kulingana na sehemu wanazofanyia kazi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sangu alisema katika kuhakikisha matumizi sahihi ya wafanyakazi wa kujitolea, serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mwongozo huo ambao utaweka utaratibu kwa waajiri/sekta na kada mbalimbali namna ya kuwapata, kuwasimamia na kuwalipa maslahi wafanyakazi watakaojitolea katika taasisi zao.

Alifafanua kuwa serikali inaruhusu waajiri mbalimbali katika utumishi wa umma kutumia wahitimu wa vyuo katika ngazi mbalimbali za elimu kufanya kazi kwa kujitolea katika maeneo yao ili kupata uzoefu wa kazi kwa fani zao.

"Kwa kuwa wahitimu hao siyo watumishi wa umma, miongozo ya kiutumishi haijaelekeza utaratibu wa kuwalipa mishahara au posho ya kujikimu," alisema.

Pamoja na maelezo hayo, alisisitiza serikali inatambua umuhimu wa wafanyakazi wanaojitolea katika utumishi wa umma.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Onyo pekee kwa waganga wa jadi halitoshi, vitendo vinahitajika zaidi

**KATIKA** miezi kadhaa, kumekuwa na taarifa za kuenea kwa ukatili vikiwamo vitendo vya utekaji wa watoto na watu wazima pamoja na ulawiti na ubakaji. Sambamba na vitendo hivyo, baadhi ya miili ya watu ikiwa imetupwa kwenye vichaka na kando ya barabara ikiwa kwenye mifuko ya sandarusi, maarufu kama viroba.

Kutokana na kuwapo kwa matukio hayo, makundi mbalimbali yamepaza sauti kutaka hatua dhidi ya washukiwa na vitendo hivyo kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Baadhi ya wanasiasa na wanaharakati pia wamepaza sauti na kusema kuna sheria zinazosimamia na kuchukua hatua dhidi ya vitendo hivyo ikiwamo kufungwa jela maisha kwa wanaothibitika kufanya hivyo.

Licha ya sauti hizo, wanaharakati na watu wa makundi mbalimbali wameiomba serikali kuchukua hatua stahiki katika kukomesha vitendo hivyo kwa kuwa vinaifanya nchi kuwa na taswira hasi katika jumuiya ya kimataifa.

Tayari serikali kupitia viongozi wametoa kauli kuhusu hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi lililopewa dhamana ya kusimamia usalama wa rai ana mali zao, limeshaanza kuchukua hatua. Wiki hii, mathalan, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam lilifanya kikao na waganga wa tiba mbadala ikiwa hatua mojawapo ya kujaribu kukomesha vitendo hivyo.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kuwaelimisha waganga hao kuhusu madhara yatokanayo na kazi zao hususan upigaji wa ramli chonganishi na kuwataka wenye tabia hizo kuacha mara moja.

Waganga hao wamekuwa wakidaiwa kufanya hivyo na kuwagombanisha watu katika familia na pia wamekuwa wakiwataka wateja wao kutoa kafara ili wafanikiwe katika biashara au kupanda vyeo kazini. Mbali na kutoa kafara, wamekuwa wakiwapa masharti wateja wao kwamba ili kufanikiwa hawana budi kufanya vitendo viovu kama vile kulawiki na ubakaji wa watoto wadogo.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Mulilo, alisema jeshi limefikia hatua hiyo ikiwa ni katika jitihada za kuhakikisha usalama na kukemea vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na wanawake vinavyojihusisha na ulawiti na ubakaji ambavyo wakati mwingine husababisha waathirika kupoteza maisha.

Hatua iliyochukuliwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam ni nzuri na ya kupongezwa kwa sababu inatoa mwanga wa kupunguza tatizo ambalo sasa limezidi kuota mizizi. Waganga wa jadi wamekuwa wakidaiwa kuwa chanzo kwa sababu baadhi ya watu huamini kwamba bila kufanya uovu ikiwamo kubaka na kulawiti tena watoto wadogo au kutoa kafara hawawezi kupata mafanikio ama ya biashara, kisiasa au kupanda vyeo kazini.

Pamoja na kwamba hatua hiyo ni nzuri, kutoa onyo pekee hakutoshi bali zinatakiwa hatua zaidi za kuwafuatilia waganga hao kuhusu matendo yao ya kila siku katika ufanyaji kazi zao. Waganga hao wanapaswa kuchunguzwa kama wanafanya ramli chonganishi na wanaobainika kuendekeza vitendo hivyo kuchukuliwa hatua ikiwamo kufutiwa leseni na kufikishwa katika vyombo vya sheria.


Badala ya kufanya vitendo hivyo ambavyo ni aibu kwa taifa, waganga hao wanapaswa kuwa na weledi katika shughuli zao kwa kuwasaidia wateja wao bila kufanya ramli chonganishi au kuwaelekeza kufanya vitendo viovu. Wanachopaswa kufanya si kufanikisha shughuli zao ili kupata fedha bali kuwaambia wateja wao kwamba mafanikio hutokana na mtu kufanya kazi na si kugharimu maisha ya mtu mwingine.

Pamoja na hayo, katika nyakati hizo ambazo kumekuwa na mafundisho mbalimbali ya dini, jamii inapaswa kufahamu kwamba ili mtu afanikiwe hana budi kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Maneno na maonyo yamekuwa mengi sasa vinahitajika vitendo zaidi kukomesha vitendo vya ubakaji, ulawiti, utekaji na mauaji dhidi ya watu wasio na hatia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Matatizo ya TAZARA yamepata dawa, magumu yaliyotokea yamefika mwisho

Na Beatrice Moses

**ABIRIA** waliotarajiwa kusafiri na treni ya Tazara kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi jirani ya Zambia 3 Septemba,2024 , walikwama na kulazimika kukaa siku mbili stesheni ya Tazara Dar Salaam

Dhahama hiyo imewakuta abiria hao waliokwama kwa siku mbili, pasipo kufahamu hatma yao, wakibaki katika wakati mgumu, ikiwamo kukosa mahali sahihi pa kujisitiri.

Ofisa Uhusiano wa TAZARA Tanzania, Regina Tarimo amekaririwa akieleza kuwa ni changamoto za kila mara, kutokana na uchakavu wa mabehewa yao, hivyo hulazimika kuyafanyia matengenezo mara nyingi.

Kwa maelezo hayo ya Afisa Uhusiano, ni wazi kwamba kuna ombwe kubwa unaosababisha maisha ya abiria kuwa hatarini. Nasema hivyo, kwa sababu kama wenye mamlaka wanajua kuna matatizo ya namna hiyo, kuna haja gani ya kuruhusu safari kuwepo?.

Huko ni kuyaweka maisha ya watu rehani katika mazingira kama hayo. Ni jambo ambalo halipaswi kufumbiwa macho. Uongozi wa Tazara kuna maswali ya kujibu.

Je kwanini mmeendelea kulazimisha safari katika mazingira ambayo mnatambua mabehewa yenu ni chakavu? Je mnajua miongoni mwa abiria mnaowahudumia wapo pia ambao ni wagonjwa wa presha au sukari? Fidia ya usumbufu ambao abiria hao wanapaswa kupewa je gharama zisingeepukwa kama msingezuia safari mapema(tiketi zisingekatwa)?

Novemba 2022 serikali kupitia kwa aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete ilisema katika mwaka wa fedha 2022/23, imetenga Sh bilioni 13.1 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika aliyetaka kufahamu mkakati wa serikali wa kukarabati reli ya Tazara.

Naibu Waziri alikaririwa akielezea kuwa ununuzi wa mtambo wa kisasa wa kushindilia kokoto, pia baadhi ya fedha hizo zitatumika kukarabati mabehewa 21 ya treni za abiria za Udzungwa na treni za abiria za mjini za jijini Dar es Salaam, je maelezo haya yaikwama wapi kutelekezwa? Kama haikutekelezwa ilikwama wapi?

Kwa upande wa mikakati ya muda wa kati na mrefu, alikaririwa akisema kuwa serikali za Tanzania na Zambia zimeandaa Mpango wa Biashara wa miaka mitano uliotarajiwa kupitishwa na Baraza la Mawaziri mwishoni mwa Novemba, 2022. serikali za Tanzania, Zambia na China zimeunda timu ya pamoja kwa ajili ya kuandaa mkakati wa pamoja kwa kuishirikisha Serikali ya Watu wa China katika kugharamia maboresho ya Tazara.

Maelezo hayo ya ushirikishwaji wa China tayari tumeona utekelezaji wake unavyoendelea baada ya juzi Septemba 4 mwaka 2024 kufanyika utiaji saini waraka wa maelewano kuhusu mradi wa Ufufuaji wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambao ulishuhudiwa na Rais wa China Xi Jinping, Rais wa Tanzania Dk,Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zambia Hakainde Hichilema.

Hii ni habari njema yenye matumaini kwa kuwa imeelezwa wazi kuwa China ipo tayari katika kushiriki kwenye hatua ya kufufua ushirikiano wa reli kati ya Tanzania na Zambia, hali ambayo inatajwa kuwa ikifanikiwa itafanikisha kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli katika eneo hilo.

Hatua hii ikifanikiwa, imani yangu ni kwamba hatutarajii tena kutokea usumbufu kwa abiria, ikiwamo hiyo ya kulazimika kulala stesheni.

## Serikali kuongeza elimu ukuzaji viumbe maji

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema inalenga kuongeza elimu ya ukuzaji viumbe maji, ukiwamo uzalishaji vifaranga vya samaki hasa kaa ili kuongeza tija, mnyororo wa thamani na kupata soko la kimataifa.

Mkurugenzi wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla, amesema wamechukua hatua hiyo baada ya takwimu kuonesha dunia imekwishapoteza uvuvi wa asili.

Madalla aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo ya siku tano kwa wanazuoni vijana takribani 40 kwenye sekta ya uvuvi, kuwapa mbinu za ukuzaji viumbe maji, vikiwamo vifaranga vya samaki, yaliyofanyika katika Chuo cha Uvuvi Mbegani (FETA), wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

“Soko la baadhi ya viumbe maji kama kambale na kaa bado ni changamoto. Samaki aina ya kambale kuna baadhi ya imani za kidini kwamba hawali samaki asiye na magamba, pia kaa soko lipo ila hatua za vitotoreshi ni duni.

“Serikali imedhamiria kujenga vituo viwili vya uzalishaji vifaranga. Duniani imebainika kuwa mwaka 2022 katika takwimu asilimia 51 ya samaki waliliwa duniani, walitoka katika mazingira ya kufuga. Tanzania pia tunajitahidi kufikia asilimia 10 ya mazao yote uvuvi yanatokana na mazingira ya kufuga,” alisema Dk. Madalla.

Mratibu wa mafunzo hayo, Lucka Mgwena, alisema lengo ni kuwajengea uwezo vijana wahitimu katika fani za sayansi ya viumbe maji (aquaculture) ngazi ya cheti, diploma na shahada ili wabaini fursa zilizopo kwenye ukuzaji viumbe hao nchini na kujiajiri.

“Vilevile, tunataka wawe na maarifa ya vitendo kwenye uzalishaji bidhaa, usimamizi na utafutaji masoko ya bidhaa zitokanazo na viumbe maji nchini. Maarifa yote yemejikita katika kuendeleza ukuzaji viumbe maji kibiashara,” alisema Lucka.

Alisema kuwa, akiwa mmoja wa wanufaika na ufadhili wa masomo katika Shahada ya Uzamili wa Ukuzaji Viumbe Maji na Sayansi ya Uvuvi kupitia mradi huo, alifikiri namna ya kuwafikia vijana wahitimu ili kuwaongezea maarifa ya kuwawezesha kuzibaini fursa na kujiajiri.

Lucka alisema, mfadhili wa mafunzo hayo ni AQUAFISH - African Centre of Excellence in Aquaculture and Fisheries (ACE II) kupitia Chuo Kikuu cha Lilongwe cha Kilimo na Maliasili (LUANAR) cha Malawi.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Dk. Kheri Kagya (wa pili kushoto), akipata maelezo ya mradi wa kisayansi unaohusu dawa ya asili ya kutibu meno na matibabu yake uliobuniwa na mwanafunzi wa Shule ya Kibutuka ya Liwale, Afidhi Maulidi (kushoto), wakati wa maonesho ya Sayansi na Teknolojia mkoani humo jana, kupitia programu ya kuwajengea uwezo wa kisayansi wanafunzi, inayotekelezwa na Shirikisho la Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST) kwa kushirikiana na Kampuni ya Shell Tanzania. Kulia ni Mshauri wa Masuala ya Kijamii wa Kampuni hiyo, Msomisi Mmbena. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanamtandao rushwa ya ngono walipongeza Bunge

**Na Mary Geofrey**

WANAMTANDAO wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania wamelipongeza Bunge kwa kutopitisha kifungu cha 10(b) cha Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono.

Pia, wamelipongeza Bunge kwa kuongeza wigo wa ukomo wa adhabu kwa waomba rushwa ya ngono kutoka miaka mitatu hadi 10 na adhabu ya Sh. milioni tano hadi milioni 10.

Pongezi hizo zilitolewa juzi mkoani Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Mtandao huo unaohusisha zaidi ya asasi 200, Prof. Penina Mlama, tamko lake likisomwa na Mwanamtandao, Mary Marandu.

Mkutano huo na waandishi wa habari ulitawaliwa na nyimbo, shangwe na vigelegele kuashiria kuunga mkono uamuzi wa Bunge la 12 kikao cha 15, kilichojibu kiu ya mtandao kwa kutopitisha kifungu hicho cha sheria.

Awali mtandao huo ulipinga kifungu hicho cha 10(b) kwa madai kinahalalisha rushwa ya ngono kwa vijana na wasichana na kumlinda mwombaji rushwa.

Badala yake, walitaka kifungu cha 25 cha sheria hiyo kibaki kama kilivyo bila marekebisho yoyote kwa kuwa kinajitosheleza.

“Wanamtandao wa Kupambana na Rushwa ya Ngono tunapenda kutumia fursa hii kupongeza wanamtandao wote, waandishi wa habari, wadau wa kimataifa waliotuunga mkono na jamii ya Watanzania kwa kusimama kidete kupaza sauti zao na kukataa mapendekezo ya kifungu hiki kilichotaka mwathirika wa rushwa ya ngono kushtakiwa kama mhalifu.

> **“Kipekee tukitambua juhudi na mchango mkubwa wa Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania, Eusebia Munuo aliyeendelea kuelimisha umma wa Watanzania...**

“Hatua ya Bunge kuridhia kutopitisha kifungu hiki na kuongeza adhabu kwa waomba rushwa ya ngono ni ushindi mkubwa kwenye mapambano dhidi ya rushwa ya ngono na uthibitisho tosha wa nguvu yetu wananchi na umuhimu wa sauti zetu kama wanajamii katika kukataa mifumo kandamizi,” alisema Mary.

Mtandao huo ulitambua mchango wa Chama cha Wanawake Majaji waliowezesha kuingizwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu Na. 25 kilichotofautisha rushwa ya ngono na rushwa zingine.

“Kipekee tukitambua juhudi na mchango mkubwa wa Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania, Eusebia Munuo aliyeendelea kuelimisha umma wa Watanzania kuhusu dhana nzima ya rushwa ya ngono,” alisema Mary. Mwanamtandao Rebeca Gyumi alisema wanatambua Sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa ya Ngono, imetoa tafsiri sahihi iliyotofautisha rushwa ya ngono na rushwa nyingine.

“Kwamba rushwa ya ngono inahusisha wenye mamlaka kutumia vibaya mamlaka yao kudai ngono kama sharti la kumpa mwathirika haki na stahiki zake au kumpendelea kwa kumwahidi kumtunuku vitu ambavyo hakustahili,” alisema Mwanaharakati huyo.

Pia, mtandao huo ulihusika na uchambuzi yakinifu wa mapendekezo ya awali ya marekebisho ya sheria hiyo na kutoa tamko lao kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# LATRA yaanzisha utaratibu wa uwakala kudhibiti ajali bodaboda

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeanzisha utaratibu wa kuwapatia uwakala wa kutoa leseni, vyama vya wamiliki na waendesha bodaboda pamoja na bajaji katika maeneo mbalimbali nchini ili kurahisisha udhibiti na uzingatiaji wa kanuni na sheria za usafirishaji katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, Salum Pazzy, kuanzishwa kwa utaratibu huo kutasaidia kundi hilo kutoa huduma bora na salama pamoja na kupunguza ajali zinazokatisha maisha ya vijana wengi na wengine kuwapa ulemavu wa kudumu.

Pazzy alisema pamoja na mambo mengine, utaratibu huo utatoa fursa kwa vyama hivyo kujipatia kipato kupitia ukatishaji wa tiketi za usafirishaji kwa wanachama wao.

"Vyama vyao vitakuwa vinatoa leseni kwa wanachama wao kwa niaba ya LATRA na watakuwa wanasimamiana au kudhibitiana wao kwa wao na tunafahamu kwamba, wanapojiwekea utaratibu hawana mchezo. Hii itaturahisishia kazi kwa kiwango kikubwa.

Alisema kundi la waendesha bodaboda na bajaji ndilo linaloonekana kuwa na shida kubwa katika kulidhibiti.

"Watajiwekea utaratibu wa kujidhibiti kupitia vituo vyao, yule ambaye hana leseni na hafuati sheria na kanuni za usafirishaji hawatamruhusu kufanya kazi, kwa hiyo watapeana msukumo wa kufuata sheria kabla serikali haijawafikia.

"Hatutaki watoe leseni ilimradi, bali kwa kuhakikisha kila anayepewa anakuwa na sifa na amefuata sheria, kanuni na taratibu za usafirishaji na tumejiridhisha katika hili, wanajitahidi na wamejipambanua kwa umoja," alisema Pazzy.


> **"Vyama vyao vitakuwa vinatoa leseni kwa wanachama wao kwa niaba ya LATRA na watakuwa wanasimamiana au kudhibitiana wao kwa wao na tunafahamu kwamba, wanapojiwekea utaratibu hawana mchezo. Hii itaturahisishia kazi kwa kiwango kikubwa.**

Alisema asilimia 20 ya fedha inayopatikana katika vikundi hivyo kupitia leseni, inatumika kuvisaidia na asilimia 80 inakwenda serikalini.

"Na ndio maana tunasema hii ni fursa nzuri kwa vijana wanaofanya shughuli hiyo, kwa sababu wanakuwa na mfuko wa fedha ambao ni ada ya leseni zao wenyewe. Kupitia utaratibu huu vyama vyao vitakua kiuchumi na kuwa na nguvu zaidi," alisema Pazzy.

Alisema tayari vikundi vya bajaji na bodaboda vya Mkoa wa Kilimanjaro vimefanya vizuri katika eneo hilo na kuwahamasisha wenzao kutoka mikoa ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha utaratibu huo unafika katika mikoa yote nchini.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. 19329 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

MPELI WILLIAM MANASE……………………ACCUSED PERSON

To:
Mpeli William Manase
Wazo Ward, Mivumoni Area, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. 19339 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

PONSIAN RWEZIMULA BAYONA……………………ACCUSED PERSON

To:
Ponsian Rwezimula Bayona
Bunju B Area, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. 19325 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

SALOME MAKAMBA……………………ACCUSED PERSON

To:
Salome Makamba
Survey Area, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

# Ubelgiji yaunga mkono ajenda ya nishati safi

**Na Halfani Chusi**

UBELGIJI imesema inaunga mkono kampeni ya Nishati Safi ya Kupikia ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ni kinara upande wa Afrika.

Ubelgiji imeonesha nia ya kushirikiana na Tanzania kutekeleza ajenda hiyo kupitia kikao kilichofanyika kati ya Naibu Waziri wa Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko na Waziri wa Nishati wa Ubelgiji, Tinne Van Der Straeten.

Kikao hicho kilichofanyika mjini Windhoek, Namibia, ikiwa ni sehemu ya mkutano wa nchi za Afrika kujadili matumizi ya Hydrojen katika kuzalisha umeme.

Waziri Tinne alisema nchi yake iko tayari kuunga mkono jitihada za matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwa ni mkakati wa kimataifa wa uhifadhi wa mazingira na kuwawezesha wananchi kukuza pato na maendeleo ya kiuchumi.

Alisema matumizi ya vyanzo mbalimbali vya nishati safi ni njia mojawapo ya kuchochea maendeleo ya watu na uchumi wa nchi husika.

Dk. Biteko alisema ili kupata maendeleo ya kweli, Tanzania inatoa kipaumbele katika matumizi ya nishati ambayo itawawezesha kupata mafanikio endelevu, ikiwa ni pamoja na kuondokana na magojwa na vifo vinavyotokana na matumizi ya nishati chafu.

"Kama mnavyofahamu, Tanzania kupitia Rais Samia imeasisi na inaendeleza kampeni kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia katika kipindi cha miaka 10 ijayo kuanzia mwaka huu," alisema.

Dk. Biteko alisema anatamani Tanzania ingeungwa mkono na Ubelgiji katika matumizi ya nishati safi kama ambavyo imekuwa inafanya katika sekta nyingine ikiwamo elimu na uwezeshaji katika masuala ya usawa wa kijinsia.

Kikao hicho kililenga kuibua fursa na changamoto zilizoko katika matumizi ya nishati hiyo, ambapo Tanzania itapata fursa ya kujifunza kuhusu matumizi yake katika kuzalisha umeme.

# Vicoba sasa wahamasishana kuwania uongozi wa mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPENI ya kuhamasisha idadi kubwa ya wanawake na vijana kuchukua fomu za kuomba kuwania uongozi uchaguzi ujao wa serikali za mitaa nchini ili kuchochea mabadiliko ya fursa za kiuchumi, imehamia katika vikundi na Benki za Kijamii Vijijini (Vicoba).

Akizungumza katika Kata ya Majengo, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na wanachama wa Vicoba wakati wa kuvunja mzunguko wa 16 wa Kikundi cha Amkeni Vicoba Group, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Tusonge (CDO), Aginatha Rutazaa, alisema umefika wakati wanawake na vijana kuwa vinara katika masuala ya uongozi.

"Sasa nataka kusema hivi, tunaingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, ajenda kubwa ya Tusonge CDO ni kuona akina mama wengi kwa kadri iwezekanavyo mnaingia kwenye nafasi za uongozi kuanzia mtaa, kitongoji na kijiji na kule kwenye kata mwaka ujao," alisema na kuongeza kuwa: "Naomba kila mwanamke kuandikisha jina lake kwenye daftari la mpiga kura. Huo ndio ufunguo wa kutusaidia kuingiza funguo kwenye gari ili liwake. Tutaongea, tutapiga kelele, tutahamasisha, lakini kama hujajiandikisha ni kama mtu anatwanga maji kwenye kihuri."

**Na bila kuwa na msingi ndani ya serikali za mitaa, hata huko juu tukaja tukapata viongozi wazuri, bado watashindwa kufanya kazi, kwa sababu utakuwa msingi...**

Alisema anatambua wanawake ni jeshi kubwa lenye mchango mkubwa kwa taifa, kwa kuonyesha uwezo wa kubeba mzigo kuanzia ngazi ya familia pasipo kuwezeshwa.

Na bila kuwa na msingi ndani ya serikali za mitaa, hata huko juu tukaja tukapata viongozi wazuri, bado watashindwa kufanya kazi, kwa sababu utakuwa msingi umenyonya maji, lakini matofali yatashindilia msingi na utavunjika," alisisitiza.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliutangazia umma na vyama vya siasa kuwa uchaguzi huo kwa Tanzania Bara, utafanyika Novemba 27 Novemba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019, Ibara 4 (1-3) (Tangazo la Serikali, Na. 571, 572, 573 na 574) la Mwaka 2024, waziri mwenye dhamana, anayo mamlaka ya kuutangazia umma na vyama hivyo tarehe rasmi ya uchaguzi.

Katika uchaguzi huo uliofanyika mwaka 2019, wanawake 4,171 tu, ndiyo walioshinda nafasi za uenyeviti wa vitongoji, sawa na asilimia 6.7, wa mitaa walikuwa 528 sawa na asilimia 12.6 na wa vijiji, wanawake 246 asilimia 2.1.




Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika akizungumza wakati wa mkutano wa hadhara katika eneo la Majengo Shimoni, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi, akiwataka wanachama wa chama hicho, kujipanga ipasavyo kushiriki uchaguzi wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# ECLEA yaahidiwa maji ya bomba

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG'

SERIKALI imeahidi kutafuta ufumbuzi tatizo la ukosefu wa maji ya bomba katika Chuo cha Masomo ya Theolojia na Uongozi Afrika Mashariki (ECLEA) kilichopo wilayani hapa Mkoa wa Manyara.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Athuman Likeyekeye, alitoa ahadi hiyo jana katika mahafali ya chuo hicho yaliyofanyika wilayani hapa.

Kwa mujibu wa Likeyekeye, tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi hivi karibuni ili kuruhusu shughuli za kitaaluma kutolewa bila vikwazo chuoni hapo.

"Tatizo la kukosekana maji hapa serikali imelisikia na italifanyia kazi kwa uharaka wake, lakini ni vizuri waende wakatende haki na kusisitiza masuala ya maendeleo na amani ya nchi," alisema.

Katika risala yao iliyosomwa na Salome Michael, wahitimu hao wameahidi kwenda kutatua migogoro ya ndoa katika jamii na kusaidia malezi ya watoto.

Katika mahafali hayo, Mkuu wa ECLEA, Ibrahim Joramu, aliwataka kutojisifia kuwa na vyeti, bali wakawe chachu ya kuleta mabadiliko katika jamii kutokana na elimu waliyoipata.

"Msiende kuonyesha vyeti tu ila matendo yenu ndio yaonyeshe elimu mliyoipata mambo mliyojifunza mkayafanyie kazi ili yazae matunda kwenye jamii," alisema Joramu

Alisema kusudi la elimu waliyoipata ni kuleta mabadiliko chanya katika jamii huku tabia zao zikiwa za pekee.

Mkuu huyo, alisema madhumuni yao ni kuleta chachu ya mabadiliko kwa wanafunzi ili nao wayapeleke katika jamii yao.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki wa ECLEA, Dk. Jonathan Menn, alisema kanisa linakuwa zuri kulingana na uzuri na ubora wa viongozi.

Menn, alisema wachungaji wengi hawajapata mafunzo ya kina kama waliyoyapata, matokeo yake wanajifunza kutoka kwa baba zao wa kiroho.

# Himo, Holili tishio uchakachuaji gesi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MIJI ya Himo Wilaya ya Moshi Vijijini na Holili wa Rombo mkoani Kilimanjaro inatajwa kuwa tishio kwa biashara ya uchakachuaji wa nishati safi ya gesi ya kupikia majumbani (LPG).

Kwa mujibu wa Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanahujumu nishati hiyo kwa kuchakachua ujazo wa mitungi ya gesi na kuuza ikiwa na ujazo pungufu.

Kuhusu uagizaji, uhifadhi, usambazaji na ujazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Long'idu, alisema ni lazima ijazwe kwa kuzingatia uzito sahihi kama unavyoonyeshwa kwenye mitungi.

"Kwa Kanda ya Kaskazini, kuna idadi ya watu ambao tumewakamata kwa sababu kuna changamoto kubwa sana ya uchakachuaji. Kwa sababu eneo hili la Kilimanjaro lina barabara inayopeleka gesi nchi jirani ya Kenya. Kwa hiyo kuna uchakachuaji hasa kwa haya magari makubwa yanayopita maeneo ya Himo, Holili (mpaka wa Tanzania/Kenya). Kuna ile hali ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wanachakachua," alisema na kuongeza kuwa: "Tumekuwa tukishirikiana na vyombo vingine vya serikali, na tumewakamata na kuna ambao tumewapeleka mahakamani, wengine wameshtakiwa na wengine kesi zao bado tunaendelea nazo.

Bado zoezi hili la kuendelea kufuatilia ni endelevu katika mikoa ya kanda ya kaskazini ya Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro, kujua nani anafanya hii biashara bila kufuata taratibu."

Ofisa Vipimo wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kilimanjaro, Yuda Thade, alisema makosa makubwa yanayotokea kwenye biashara ya gesi ni wafanyabiashara kutokuwa na mizani.

Kwa mujibu wa Thade, makossa hayo ni kuuza gesi ikiwa na uzito pungufu, kinyume na kifungu cha 41 cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340, na kuuza gesi ambayo mtungi haujaandikwa, kinyume na kifungu cha 3 na 4 cha Kanuni za Mwaka 2013.

Kosa la kutumia mizani ambayo sio sahihi, iliyochezewa au kutothibitishwa, kinyume na kifungu cha 35 na 36 cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340, adhabu kwa mujibu wa sheria, kifungu cha 45, kwa kosa la kwanza, faini isiyopungua ni shilingi 300,000 na isiyozidi milioni 50, au kifungo gerezani si zaidi ya miaka miwili, au vyote kwa pamoja.

Kwa kosa la pili, faini isiyopungua 500,000 na isiyozi shilingi milioni 100, au kifungo gerezani, si zaidi ya miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja.







Katibu Tawala Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza, Mariam Msengi (kulia) akikabidhi kadi za bima ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa) kwa moja ya familia kutoka Kata ya Sangabuye juzi, zilizotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la SOS Children's Village Tanzania kwa wananchi zaidi ya 360 kutoka kaya maskini. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Madiwani wapinga ununuzi 'shangingi' la mkurugenzi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MADIWANI wa Halmashauri ya Tarime Vijijini mkoani Mara wamepinga kiasi cha Sh. milioni 110 kuongezwa kwa ajili ya kumnunulia mkurugenzi wa halmashauri hiyo gari aina ya Toyota Land Cruiser VX na kuagiza kutumika kwa ajili ya matengenezo ya magari mabovu ili yatumike kwenye kazi husika.

Madiwani hao, walitoa pingamizi hilo juzi katika kikao cha baraza lao kilichokuwa kikijadili matumizi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mmoja wa madiwani hao, na baadhi ya madiwani hao, Johnbosco Mbusiro, alisema matumizi ya fedha hizo ni mabaya na kutaka kuelekezwa katika utekelezaji wa miradi mingine muhimu ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi na serikali.

Diwani Nashoni Mchuma, alisema miradi mingi imekwama na kuitaja baadhi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Afya Susuni na vyumba vya madarasa hivyo kutaka fedha hizo zielekezwe huko. Vilevile Mchuma, alitaka fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi Ng'ereng'ere zaidi ya Sh. bilioni moja zipelekwe kuanza ujenzi huo na kukamilika kwa wakati na kuwaondolea kero wananchi.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Solomon Shati akizungumzia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, alisema zinatarajiwa kutumika zaidi ya Sh.milioni 448.4 kwa miradi, ikiwemo ujenzi wa mabweni mawili ya Shule ya Sekondari ya Wasichana kidato cha tano na sita ya Borega.

Vilevile alitaka kukamilishwa kwa ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha afya Magoto, ujenzi wa madarasa mawili ya watoto wenye mahitaji maalum, ununuzi wa vishikwambi na gari hilo ambao ulipingwa na madiwani hao.

# Wananchi waitwa kupima homa ya ini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wametakiwa kujitokeza katika vituo vya afya kupima afya ili kubaini kama wameambukizwa ugonjwa wa homa ya ini.

Wito huo ulitolewa juzi Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Athuman Matindi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusiana na wanavyohamasisha wananchi kupima afya zao mara kwa mara ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukizwa na yasiyo ya kuambukiza hasa wa homa hiyo na Virusi vya Ukimwi (VVU).

Dk. Matindi, alithibitisha kuwepo kwa wagonjwa watatu wa homa hiyo katika familia moja baada ya kupimwa Kituo cha Afya Burungwa na kuwataka wakazi hao kujitokeza na kupima afya zao na kupatiwa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo na mengine.

Alisema utafiti unaonyesha virusi vya homa hiyo vinaweza kuishi nje ya mwili hadi siku saba, vikiwa na uwezo wa kuambukiza mtu.

Alitaja makundi yaliyopo hatarini kupata ugonjwa huo kuwa ni watoto wachanga waliozaliwa na mama mwenye virusi hivyo, wanaofanya ngono, wanatumiaji dawa za kulevya, wafanyakazi wa sekta ya afya na wagonjwa wa figo wanaotumia huduma za kusafisha damu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala, aliwataka watoa huduma ngazi za jamii kushirikiana na mashirika yaliyopo kuelimisha wananchi umuhimu wa kupima afya na kueleza madhara ya magonjwa hayo.

Mkazi wa Nyamilangano, Msanja Masasila, alisema wananchi wengi hawana elimu ya ugonjwa huo na kwamba wengi wao wana imani potofu juu ya wagonjwa hao wakidhani wamerogwa na kukimbilia kwa waganga wa jadi kupatiwa tiba asili.

# RC Simiyu awakumbusha wananchi uboreshaji taarifa daftari mpigakura

**Na Alex Sayi,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Kenan Kihongosi amewataka wananchi wenye sifa kuendelea kujitokeza katika vituo vya kujiandikisha pamoja na kuboresha taarifa zao katika daftari la kudumu la mpiga kura.

Kihongosi alitoa kauli hiyo juzi ofisini kwake na kueleza kuwa kwa wote wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea wana sifa za kushiriki katika uandikishaji huo unaoendelea ili kuwa na sifa za kushiriki Uchaguzi Mkuu.

Mratibu wa daftari la kudumu ngazi ya Kata, Dk. Boniphas Mabonesho alisema uelewa, mwamko na mwitikio bado upo chini, hivyo aliwaomba wasimamizi kuongeza hamasa zaidi.

"Mimi naratibu kata sita za Shanwa, Nyalikungu, Binza, Mwamashimba, Sola na Ng'wigwa uhamasishaji unaendelea vizuri lakini bado kunahaja ya hamasa hiyo kufahamika kwa wananchi wote ili waweze kujitokeza kuboresha taarifa zao hasa kundi la vijana," alisema Dk. Mabonesho.

Baadhi ya vijana wakiwemo waendesha daladala za baiskeli wilayani Maswa wakizungumza na Nipashe walieleza kutokuwa na uelewa wala elimu sahii juu ya suala la kuboresha na kujiandikisha katika daftari hilo.

Issack Joseph (18) Mkazi wa Kata ya Sola alisema anahitaji kujiandikisha lakini hakuwa na taarifa licha ya kitambulisho hicho kuwa na faida katika shughuli mbalimbali.

# Vijana 300 wawezeshwa ujuzi kujiajiri kwa kilimo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa ajira kwa vijana nchini, zaidi ya vijana 300 wamepatiwa ujuzi pamoja na vifaa ili kujiajiri katika kilimo na ufundi.

Vijana hao wanaojishughulisha na kilimo cha umwagiliaji, ufundi umeme pamoja na ufundi wa nguo wameeleza kurejesha matumaini yao kufuatia msaada huo walioupata kutoka shirika lisilo la kiserikali la SOS Children's Village Tanzania.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi vifaa kwa vijana 35 kutoka kata mbili za Wilaya ya Ilemela, Meneja wa SOS Children's Village Tanzania Mkoa wa Mwanza, John Masenza alisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za haraka kukabiliana na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana.

"Hawa ni miongoni mwa vijana walioshindwa kutimiza ndoto zao za kielimu lakini pia hawana njia mbadala ya kujipatia kipato, hivyo tumeamua kuwapa mashine za kushona nguo, vifaa vya kisasa vya kilimo cha umwagiliaji pamoja na mbegu za kisasa ili kuwawezesha kujipatia kipato na kuinua maisha yao," alisema Masenza.

Masenza alisema shirika hilo limekabidhi kadi za bima ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa) 360 kwa kaya masikini ili kuzisaidia kumudu huduma za matibabu.

Mkulima wa bustani za mboga, Philpo Joseph, alisema mbinu za elimu ya kilimo walizopatiwa pamoja na zana za kisasa zitamsaidia kutoka kwenye kilimo cha mazoea kwa kutumia mashine walizopatiwa ili kuongeza uzalishaji na kujiinua kiuchumi.

Mhitimu wa mafuzo ya ushonaji nguo, Evodia Martine, alisema kazi hiyo inamsaidia kuendesha maisha yake pamoja na familia kwa ujumla.

Katibu wa Wilaya ya Ilemela, Mariam Msengi, alipongeza juhudi hizo na kuwashauri wanufaika kutumia vyema zana na mafunzo walivyopewa.



Ukurasa 13

Vita vya mauaji, ubakaji, ulawiti wasiachiwe polisi pekee yao



## EWURA NA MAJIBU UKAMILISHAJI SDG 2030 KATIKA MTAA WAKE

Ukurasa 14


# BUFE


IJUMAA SEPTEMBA 6, 2024

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe


# Undani wa Samia, Hichilema 'kuifufua' TAZARA kwa mwezeshaji wao China

- Yaleyale ya Nyerere, Kaunda na Mao
- Bandari Dar, shaba Zambia kupaishwa
- Kuna bandari kavu, umeme unapelekewa
- Biashara mahindi sokoni Sh. bilioni 650



Marais Hakainde Hichilema wa Zambia, Dk. Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wao, Rais Xi Jinping wa China, walipokutana katika kikao cha faragha, kwenye Mkutano wa Ushirikiano Kati ya Afrika na China wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

**Na Peter Orwa**

WIKI hii inahesabika neema mpya katika mafanikio ya utawala wake Rais Dk. Samia Suluhu, akiingiza rekodi mpya ya maendeleo, pale unapohusishwa mradi mkubwa wa nchini, njia ya usafiri ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) uliokuwa unalega.

Mwanzo wa wazo la ujenzi ulikuwa mwaka 1968, ukaanza miaka miwili baadaye, kisha huduma zikaanza kufanyika, 1976.

Hapo kuna zao la ubunifu na urafiki kati ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, swahiba wake kisiasa, kijamii na kiitikadi, jirani Rais Kenneth Kaunda wa Zambia na komredi wao, Mao Tse Tung wa China.

Serikali ya Mao Tse Tung, ilitoa mkopo usio na riba kwa mradi huo wa marafiki, wajenzi wakitoka China. Hivyo, kinachofanyika sasa katika Serikali ya Awamu ya Sita, ni mwendelezo wa maono yaliyoibuliwa na Nyerere, miaka saba baada ya uhuru, leo ikielekea mwaka wa 67 wa maadhimisho hayo.

Ni mtazamo uleule uliowasilishwa hivi karibuni katika safu hii, Serikali ya Awamu ya Sita, inavyoendeleza mashirika ya umma, kwa mwongozo wa Mwalimu Nyerere, ila mahitaji ya sasa.

Hadi sasa nchini kuna miradi mikubwa ya namna hiyo inayoendelezwa ya Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, ambalo ni wazo la Baba wa Taifa, aina yake ya fikra ikiendelezwa katika reli nchini.

Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) ulioasisiwa kwa maono ya Serikali ya Awamu ya Nne, wote wakiwa waumini wa itikadi ya serikali ya Nyerere na dira yake.

Wakati mradi wa reli ya TAZARA ilianza kutumika mwaka 1976, ulikuja na sifa iliyoko leo ya mradi unaondelezwa kwa jina la Reli ya Kisasa (SGR), ambayo upana wa reli unazidi ule mkongwe Reli ya Kati ya TRC.

Pia, ujenzi wa sakafu yake imetandikwa nguzo za zege na kokoto nyingi, tofauti na ile kongwe yenye nguzo chuma ambayo reli yake pia nyembamba kulinganisha na SGR inayotajwa imara na salama zaidi; Reli ya TRC ilijengwa mwaka 1905 na kazi ya upimaji ilianza 1894, katika Utawala wa Koloni la Kijerumani.

Wiki hii China, Tanzania na Zambia zimetia saini makubaliano ya awali kuifanyia matengenezo reli ya Tanzania hadi Zambia kukilengwa kuboresha usafirishaji katika ukanda huo wenye utajiri wa rasilimali.

Wakati mkataba wa awali ulihusisha wazee; Mao Tse Tung, Nyerere na Kaunda, wa sasa ni marais wa Zambia, Hakainde Hichilema na Dk. Samia, na mwenyeji Rais Xi Jinping wa China, wote wakihudhuria Mkutano wa Ushirikiano Kati ya Afrika na China.

Mradi wa kwanza wa TAZARA, reli yenye urefu wa kilomita 1,860, ulijengwa kati ya mwaka 1970 na 1975 kwa mkopo usio na riba kutoka China, malengo ni kusafirisha mizigo kutoka migodi ya madini ya shaba na kobalti ya Zambia hadi bandarini, Dar es Salaam, Tanzania.

Ujenzi huo ulihusisha madaraja mengi, njia za chini na mapango, ikijumuisha wafanyakazi wa China zaidi ya 20,000 na wenyeji wa nchi hizo mbili.

Mradi wa TAZARA unaunganisha huduma ya abiria na mizigo kati ya bandari ya Dar es Salaam na kituo cha New Kapiri Mposhi, iliyopo kwenye njia ya reli kati ya Lusaka na Kitwe, ukanda wa shaba wa Zambia, ukichangia uhusiano wa kiuchumi na kibiashara kati ya nchi hizo.

Kisiasa, ililenga usafirishaji shaba ya Zambia wakikwepa bandari za Afrika Kusini iliyokuwa na serikali ya kibaguzi, pia Msumbiji, ilipokuwa koloni la Ureno.

China ikaunga mkono kwa kuwekeza katika uhusiano na msimamo huo wa mataifa huru ya Afrika, ikajitolea kudhamini mradi uliowezesha Zambia njia nyingine ya kufikia bahari.

Reli hiyo inatajwa ilipoanza kazi mwaka 1976, ilikuwa na vichwa 120 na mabehewa zaidi ya 2,000, sasa zinakadiriwa ni wastani wa vichwa 30 na mabehewa 100, huku hali ya reli na mtaji wa shirika si mzuri.

Ni njia inayopita kati ya misitu mapori, mapango makubwa na ya kuvutia nchini katika mikoa ya Kusini, Tanzania.

**VITUO MUHIMU TAZARA**

- Dar es Salaam
- Kidatu (kiungo na Shirika ya Reli Tanzania kwenda Kilosa na Dodoma)
- Ifakara
- Mlimba
- Makambako
- Mbeya

Inaendelea Uk 12

## UCHUMI

# Serikali katika operesheni kufikia mapinduzi ya uzalishaji samaki, kuanzia vifaranga wake

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi zilizozungukwa na maji ya asili, hasa Bahari ya Hindi ambayo ni chanzo kikuu cha uchumi unaopewa jina 'uchumi wa buluu'.

Sasa serikali inatarajia kuunda meli kubwa ya kisasa yenye urefu wa mita 39 maalumu kwa uvuvi wa kibiashara.

Bahari ya Hindi ni ya tatu kwa ukubwa duniani ikichukua asilimia 20 ya uso wa dunia na kuzungukwa na mabara manne. Tanzania ni miongoni mwa nchi wanufaika wa bahari hiyo.

Mkurugenzi wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla, anasema hatua hiyo ni baada ya takwimu kuonyesha dunia imekwishapoteza uvuvi wa asili, kutokana na viumbe maji kupungua kutokana na mahitaji.

Anasema, kwa sasa mikakati ni kuongeza uzalishaji wa vifaranga wa viumbe hao, kwa aina tofauti kama vile samaki na kaa, ili kukuza biashara katika soko la ndani na nje.

Mgalula Lyobah, Ofisa Mkuu wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), anasema shirika linatarajia kuanza shughuli baada ya kuanza kukarabatiwa, kuja na zana za kisasa za uvuvi zitazofika bahari kuu, ili kukidhi mahitaji ya kitoweo hicho.

TAFICO, ni taasisi ya umma iliyoanzishwa mwaka 1974 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 na ina jukumu la kuendeleza sekta ya uvuvi nchini kupitia uwekezaji katika miradi mbalimbali inayolenga kuongeza



Mkurugenzi wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla (katikati), akiwa na wanazuoni vijana 40 katika sekta ya uvuvi, walioshiriki mafunzo ya kuendeleza viumbe maji yaliyofanyika katika Chuo cha Uvuvi Mbegani (FETA), Bagamoyo mkoani Pwani. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

tija hasa katika uvuvi wa bahari kuu na kuimarisha mnyororo wa thamani kwa mazao ya uvuvi.

Inafanya shughuli zake katika ukanda wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na maji madogo.

Kwa mujibu wa Dk. Madalla, matumizi ya kila mtu ya kilo 10.5 kwa mwaka bila kujumuisha mahitaji ya mauzo ya nje ambayo ni asilimia 10 ya jumla ya uzalishaji.

Mahitaji ya samaki ifikapo mwaka 2050 inakadiriwa kufikia tani milioni 1.36 kwa makadirio ya watu milioni 129 ifikapo mwaka huo.

Dk. Madalla, anasema hatua mbalimbali zinachukuliwa baada ya takwimu kuonyesha dunia imekwishapoteza uvuvi wake katika vyanzo vya asili, kama vile bahari, maziwa na mito na mwelekeo ni katika kufuga viumbe hao.

**VIFARANGA SAMAKI**

Katika mafunzo ya siku tano kwa wanazuoni vijana 40 kwenye sekta ya uvuvi, Dk. Madalla anasema lengo ni kuwapa mbinu za ukuzaji viumbe maji, ikiwamo vifaranga vya samaki yaliyofanyika chuoni.

"Serikali inalenga kuongeza elimu ya ukuzaji viumbe hai, ikiwamo uzalishaji wa vifaranga vya samaki hasa kaa, ili kuongeza tija, mnyororo wa thamani na kupata soko la kimataifa.

"Soko la baadhi ya viumbe maji kama kambale, kaa bado ni changamoto. Samaki aina ya kambale inatokana baadhi kuwa na imani za kidini kwamba hawali samaki asiye na magamba, pia kaa soko lipo, ila hatua za vitotoreshi ni duni.

"Serikali imedhamiria kujenga vituo viwili vya uzalishaji wa vifaranga. Duniani imebainika mwaka 2022 katika takwimu asilimia 51 ya samaki walioliwa duniani, walitoka katika mazingira ya kufuga. Tanzania pia tunajitahidi kufikia asilimia 10 ya mazao yote ya uvuvi yanatokana na mazingira ya kufuga," anasema Dk. Madalla.

Mratibu wa mafunzo hayo, Lucka Mgwena, anasema lengo ni kuwajengea uwezo vijana wahitimu katika fani za sayansi ya viumbe maji (Aquaculture) ngazi ya cheti, diploma na shahada, ili waweze kubaini fursa zilizopo kwenye ukuzaji viumbe hao nchini na kujiajiri.

"Vile vile, waweza kuwa na maarifa ya vitendo kwenye uzalishaji wa bidhaa, usimamizi na utafutaji wa masoko ya bidhaa zitokanazo na viumbe maji nchini. Maarifa yote yemejikita katika kuendeleza ukuzaji viumbe maji kibiashara," anasema Lucka.

Anasema akiwa mmoja wa wanufaika na ufadhili wa masomo katika Shahada ya Uzamili wa Ukuzaji Viumbe maji na Sayansi ya Uvuvi, kupitia mradi huo, alifikiri namna ya kuwafikia vijana wahitimu, ili kuwaongezea maarifa ya kuwawezesha kuzibaini fursa na kujiajiri.

Lucka aliongeza kwamba, mfadhili wa mafunzo hayo ni AQUAFISH - African Centre of Excellence in Aquaculture and Fisheries (ACE II), kupitia Chuo Kikuu cha Lilongwe cha Kilimo na Maliasili (LUANAR) cha nchini Malawi.

Lyobah anasema, wakati dunia inaelekea katika uvuvi wa viumbe hai waliofugwa, kutokana na kupungua kwa viumbe hao katika vyanzo vya maji ya asili kama vile bahari, maziwa na mito, sasa mwelekeo ni ufugaji viumbe hao kwenye mabwawa na pembezoni mwa maji ya asili.

"Tunahitaji ufugaji wa kibiashara sio ule wa mazoea. Kuna mpango wa miradi tisa, imeanza kutekelezwa mwaka jana. Tunajenga meli kwa urefu unaoutaka, itajengwa kwa siku 270 ikiwa mita kama 39 kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu.

"Pia tuna lengo la uchakataji wa uvuvi tuwe na kiwanda, magari ya usafirishaji, tunataka kukarabati chumba cha 'cold room' tayari tuna mtambo wa barafu za chenga na tuna mtambo wa tani milioni 10 na tunatarajia kuwa tunazalisha chakula cha samaki wafugwao kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 30 kwa siku," anasema Lyobah.

Anasema changamoto ya upatikanaji wa chakula kwa ajili ya viumbe maji hasa samaki inatokana na uhaba wa malighafi sokoni amabayo inagombewa na watumiaji kama vile binadamu na wafugaji.

"Mahindi hayo hayo yanategemewa na binadamu, ikizalishwa pumba inahitajika kwa ajili ya mifugo mingine pia kama kuku. Ujenzi wa kiwanda cha

Inaendelea Uk 14

# UNDANI WA SAMIA, HICHILEMA 'KUIFUFUA' TAZARA KWA MWEZESHAJI WAO CHINA

Inatoka Uk 11

- Tunduma (Tanzania)
- Kasama (Zambia)
- Mpika
- Serenje
- New Kapiri Mposhi - kiungo na reli ya Zambia

**SAMIA KIKAONI**

Rais Dk. Samia yuko China, kwenye mkutano uliofunguliwa juzi na Rais Xi Jinping, mwenyeji wa viongozi 25 wa Afrika, hoja yake ni kuwashawishi Waafrika wanunue bidhaa nyingi za nchini mwake, kwa ahadi ya kuwapa misaada na uwekezaji zaidi.

China, inataka kupunguza uwekezaji kwingine na kuboresha uhusiano wake na nchi zinazoendelea ikiwano mikopo, pia kujikita kuwekeza kwenye miradi midogo, badala ya mikubwa ya miundombinu.

Hadi sasa kampuni nyingi za China zimewekeza katika kandarasi za ujenzi nchini, pia bidhaa zake za matumizi ya kawaida zimetawala soko nchini.

Rais Dk. Samia, kama inavyozoeleka katika vikao vingi vya maendeleo kimataifa anavyohudhuria, akatarajiwa kuhutubia mkutano huo wa Tisa, kunatarajiwa kutoa mwelekeo wa ushirikiano kati ya China na Afrika, hasa baada ya janga la corona.

Pia, unafanyika wakati ambapo msuguano wa kisiasa unazidi kuongezeka katika ngazi ya kimataifa, mathalani vita vya Russia na Ukraine, pia nyingine nyingi Afrika kama mapigano ya ndani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Viongozi wa Afrika, nao wanatafuta suluhisho la haraka la madeni yanayozidi kuongezeka barani humo, uwekezaji kuhakikishiwa miradi iliyoahidiwa katika mkutano wa mwaka 2021, Dakar, Senegal.

**BANDARI KAVU**

Mnamo Oktoba mwaka jana, Rais Dk. Samia, akatangazwa kutengwa ardhi ya hekta 20 kwa jirani yake Zambia, eneo la Kwala mkoani Pwani, kujengea bandari kavu, kufufua mazingira ya kibiashara na usafiri wa reli, TAZARA.

Ni hatua iliyochukuliwa, huku utendaji wa reli ya TAZARA inayomilikiwa na pande zote mbili, ulega, Rais akitaja shabaha ni kuharakisha usafirishaji mizigo inayopitia Bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa kwa barabara hadi sehemu mbalimbali nchini Zambia.

Vilevile, hivi karibuni serikali ilizindua bandari ilyopanuliwa ziwani na barabara kujengwa mkoani Rukwa, inayounganisha usafiri kati ya Tanzania na DRC.

Hilo linatokea, huku takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Mamlaka ya Mapato (TRA) mwaka jana, zikaonyesha mwaka 2022, Tanzania iliingiza nchini bidhaa za Zambia zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 91, huku kiwango ilichosafirisha kwenda huko ni dola milioni 80.

Mwaka 2018, Dk. Samia akiwa Makamu wa Rais, serikali ilizindua ujenzi wa Bandari kavu Inyala, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, akiufafanua ni nguzo muhimu ya ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na nchi zinazopakana nazo upande wa Nyanda za Juu Kusini, ikiwamo Malawi na Zambia.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, kwenye ziara ya Makamu wa Rais Dk. Samia, alipotembelea Bandari ya Itungi katika Ziwa Nyasa, kukagua ujenzi wa meli ya MV Mbeya II.

Makalla akasema ujenzi wa bandari kavu Inyala ulitegemewa kufanya mageuzi ya usafirishaji mizigo nchini, kupitia reli ya TAZARA ambayo ina gharama nafuu, kuliko barabara inayotumika zaidi sasa.

"Makamu wa Rais (Dk. Samia wakati huo), ujenzi wa bandari kavu Inyala ni nguzo muhimu katika ukuaji wa kiuchumi wa mkoa wa Mbeya na taifa kwa ujumla, kwani itasaidia kusogeza huduma za bandari toka Dar es Salaam hadi Mbeya hali itakayowapunzia gharama za usafiri wateja wetu wa nchi za Malawi, Zambia na Kongo," akatamka Makalla, miaka sita iloyopita.

**UMEME TZ KUTUA ZAMBIA**

Mwaka jana serikali ilitangaza mradi wa upatikanaji umeme mikoa mitano nchini, kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere, uliambatana na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Kilovoti 400 kutoka Iringa-Zambia (TAZA) na ulianza kutekelezwa Januari mwaka jana, kukitarajiwa kukamilika Janauri mwakani.

Aliyekuwa Waziri wa Nishati, January Makamba, akasema kuna eneo panajengwa Kituo cha Kupoza umeme eneo la mpakani Tunduma wilayani Momba, mkoa wa Songwe na kuna vingine vinne kama hivyo viliarajiwa kujengwa.

Mratibu wa Mradi huo. Mhandisi Elias Makunga, akasema ungetekelezwa kwa Sh. trilioni 1.4 ambazo serikali ilikuwa nazo na itakuwa kiunganishi cha kwanza cha umeme wa juu kati ya nchi Wanachama wa Kusini mwaka Afrika (SAPP)na Nchi Wanachama wa Mashariki mwa Afrika (EAPP), hali itakayochagiza biashara ya umeme, kwani Tanzania itaweza kununua umeme nje ya nchi pale panapokuwa na upungufu, pia itaweza kuuza nje pale inakuwa na ziada.

**VYAKULA KUUZWA**

Mnamo Juni mwaka huu, Tanzania imeingia makubaliano ya kuuzia Zambia tani 650,000 za mahindi, kusaidia taifa hilo kutokana na ukame unaoikumba.

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, mkataba huo unatekelezwa kwa kipindi cha miezi nane na utaiingizia Tanzania Dola Milioni 250 sawa na Sh. bilioni 650 za Kitanzania.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akaihakikishia Zambia kuwa mahindi hayo watayapata kwa wakati bila vikwazo vyovyote.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Vita vya mauaji, ubakaji, ulawiti wasiachiwe polisi pekee yao






NA ADAM FUNGAMWANGO

KUMEKUWA na matukio mengi yasiyo ya kwaida nchini kwa siku za hivi karibuni ambayo yameonekana kuwashangaza wengi.

Matukio hayo ni kama utekaji, mauaji, ubakaji, ulawiti, ambapo kila kukicha inakuwa afadhali ya jana.

Pamoja na vyombo vya habari kuandika na kufichua maovu hayo, ikitarajia kuwa na watu wataogopa, lakini ndiyo kwanza hali inazidi kuwa mbaya.

Watu wametekwa na hawajulikani walipo, maiti na viungo vya binadamu kukutwa kwa waganga wa kienyeji, baba zima linalawiti na kunajisi watoto, hizi ni habari ambazo kama zinataka kuwa za kawaida hapa nchini.

Cha ajabu ni kwamba hata hao wanaobaka, wengine wanafanya hivyo kwa watoto zao wa kuwazaa.

Kusema kweli hali hii imekuwa ya kushangaza sana na haijulikani kuna kitu gani kimetokea kwa siku za hivi karibuni.

Majuzi, Jeshi la Polisi Kanda Maalum lilikutana na waganga wa tiba mbadala na kuwaonya kuacha kufanya ramli chonganishi kwa wateja wao na kuacha kuwapa masharti wateja wao kuwa ili wafanikiwe wanatakiwa wajihusishe na vitendo vya ubakaji na ulawiti hasa kwa watoto.

Kamanda wa Polisi kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Jumanne Muliro, aliwaonya kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya waganga hao wanaofanya ramli chonganishi na zenye madhara kwa wengine.

Kwanza nitoe pongezi kwa Jeshi la Polisi kwa kuwa mstari wa mbele kutaka kutatua suala hilo. Hapa inaonyesha kuwa polisi haitaki tu kuwa na kazi ya kukamata watu wanaofanya tukio ili kuwapeleka mbele ya sheria kama ambayo kazi yao ilivyo, lakini wakaenda hatua nyingine mbele ya kutaka kuzuia matukio hayo yasijitokeze.

Pamoja na hayo, kazi ya polisi haitokamilika kwa asilimia zote kama jamii nayo haitoisaidia ili kukabiliana au kumaliza tatizo hili.

Niseme tu kuwa mambo haya yote yanaanzia ndani ya jamii yenyewe ambayo ndiyo inasababisha ya yakishatokea lawama inakuwa na vyombo vingine.

Nadhani ifike wakati jamii ijiangalie kwa kile ambacho inakifanya. Inashangaza kuona karne hii ya 21, bado watu wanaamini uganga na ulozi, badala ya teknolojia, kufanya kazi kwa bidii na kuomba Mungu.

Watu wengi kwa sasa wamesoma, lakini bado elimu yao imekuwa haiwasaidii kwani bado wanakuwa wanaamini njia za mkato za kupata kile wanachokitafuta.

Binadamu wa sasa wanapenda kufanikiwa kwa njia ya mkato, kimiujiza, bila kutumia njia ambazo zinakubalika na kuelezeka, ambazo hata mtu akikuuliza mafanikio yametokana na nini unaweza kumtajia.

Tumekuwa na kizazi ambacho hakitaki shida, hakitaki kuvumilia na kufanya kazi kwa bidii na kufanikiwa taratibu, badala yake kinachotaka kupata kazi kwa haraka, na mtu akiingia kazini miezi miwili tu awe na nyumba, gari na mshahara, mnono, akifanya biashara yake, faida iwe asimilia 300 ya mtaji wake, yaani mradi mafanikio ya haraka ndiyo wanayosababisha yote haya.

Ifike wakati jamii irudi kwenye misingi ya kawaida ya kujua kuwa duniani hakuna kitu chochote rahisi kama tunavyodhani.

Kuua mtu, kuchukua viungo, siyo dawa ya kupata mafanikio, utajiri, kazi, cheo, badala yake ni kupata laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Viongozi wa dini, jamii na wazazi turejee na kuanza kuwafundisha watoto wetu misingi ya maisha kama ilivyokuwa zamani ambapo pamoja na kwamba hakukuwa na elimu sana, walikuwa na imani na waliamini kufanya kazi kwa bidii kutumia vipaji na uwezo wao.

Tiba asili walifanya kwa ajili ya kujitibia tu kwa magojwa na si kudhuru wengine au kuwapatia maisha mazuri kwa njia ya mkato.

UCHUMI

# EWURA NA MAJIBU UKAMILISHAJI SDG 2030 KATIKA MTAA WAKE

**Na Augusta Njoji , DODOMA**

LENGO namba sita la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2030 linasisitiza kuwapatia wananchi maji safi na salama na usafi wa mazingira.

Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini zimepewa jukumu kisheria la kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama lakini kuzingatia usafi wa mazingira ikiwamo uondoshaji wa majitaka.

Hata hivyo, uondoshaji wa maji taka umeonekana bado ni tatizo linalozikabili mamlaka hizo nchini ambapo ripoti ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka 2022/23, iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inaonesha Mamlaka 21 kati ya 85 sawa na asilimia 24.7 ndio zilikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na tope kinyesi.

Mamlaka hizo ni Arusha, Dodoma, Moshi, Morogoro, Mwanza, Iringa, Songea, Mbeya, Tabora, DAWASA, Sumbawanga, Bukoba, Geita, Kigoma, Musoma, Kahama, Shinyanga, Lindi, Nzega, Sengerema na Busega.

Hali hii inaisukuma EWURA kuja na Mwongozo wa Usimamizi wa Usafi wa Mazingira na topekinyesi pamoja na mfumo uliboreshwa wa uwasilishaji wa taarifa kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira unaolenga kulinda afya na mazingira nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk.James Andilile, anasema tathmini na tafiti zilizofanywa karne ya 19 ilithibitika watu wanapokaa kwenye mazingira safi afya zinakuwa imara na kujikinga na magonjwa mengi.

Anasema idadi ya wateja wanaopata huduma ya majitaka kupitia mtandao wa bomba ilifikia 56,899 kwa mwaka 2022/23 kutoka 55,996 katika mwaka wa fedha 2021/22.



Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk.James Andilile. **PICHA: AGUSTA NJOJI.**

Anaeleza kuwa kwa kipindi hicho asilimia 97.72 ya kaya zilizo ndani ya maeneo ya huduma ya mamlaka za maji zilikuwa na vyoo na asilimia 1.32 hazikuwa na vyoo. Aidha, asilimia 0.96 ya kaya zilipata huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao wa majitaka.

Anasema EWURA imekuja na mwongozo huo unaolenga kulinda mazingira na umezingatia malengo endelevu yanayolenga kuhakikisha kunakuwapo na uwiano mzuri wa watu wanaotumia huduma salama za maji na usafi wa mazingira ikiwamo ya kunawa mikono kwa sabuni na maji.

"EWURA imeona ni muhimu kuendelea kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti huduma za topekinyesi zinazotolewa kwa wananchi ambao hawajaungwa kwenye mtandao wa majitaka ndani ya maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Maji, ili kulinda afya za watu na mazingira."

"Katika kuzingatia hili, EWURA kwa kushirikiana na Deutsche Gesellschaftfür Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH imeandaa Mwongozo huu wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na Tope kinyesi kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira,"anasema.

Anaeleza kuwa mwongozo huo umekusudiwa utumiwe na EWURA pamoja na Mamlaka za Maji katika kutekeleza majukumu yao yanayohusu huduma za majitaka na tope kinyesi kwa wananchi walio nje ya mtandao wa majitaka.

Anasema mwongozo huo unaangazia sera, sheria na muundo wa udhibiti kuhusu masuala ya udhibiti na utoaji huduma za usafi wa mazingira nje ya mtandao wa majitaka.

Katika hotuba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko kwenye kongamano la kwanza la kitaifa la usafi wa mazingira, anapongeza EWURA kwa hatua hiyo kwa kuwa changamoto za usafi wa mazingira zinahitaji suluhisho la pamoja.

"Ni dhahiri kwamba bado tuna changamoto kubwa katika eneo hili, vilevile kuna udhaifu wa kitaasisi kudhibiti ufuatiliaji na usimamizi katika mnyororo wa huduma za usafi wa mazingira kwa wasiotumia mtandao wa majitaka pamoja na ushirikishwaji duni kwa sekta binafsi kutoa huduma za usafi wa mazingira,"anasema.

Anasema ni wakati umefika wa kutumia teknolojia sahihi zinazoendana na wakati na kuchangia katika usimamizi salama wa usafi wa mazingira.

Anabainisha kuwa ili kujenga jamii yenye afya na mazingira salama kwa kizazi cha sasa na kijacho ni muhimu kuchukua hatua madhubuti kuleta mabadiliko chanya.

"Niipongeze EWURA kwa kuja na mwongozo huu wa Kiswahili ambao unalenga kuziongoza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira katika kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira ikiwamo huduma ya usimamizi wa tope kinyesi kwa wananchi walio nje ya mtandao wa majitaka,"anasema.

Aidha, anapongeza EWURA kwa kuboresha mfumo wa uwasilishaji taarifa za mamlaka hizo ambao utatoa fursa ya kuongeza takwimu zaidi kuhusu usafi wa mazingira zitakazosaidia kwenye mipango ya maendeleo hususan sekta ya maji, afya na mazingira.

"Mwongozo huu unawalenga wadau wengine kama mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi zinazotoa huduma ya usafi wa mazingira kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa majitaka, Wizara zenye dhamana, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA),"anasema.

Anafafanua kuwa takwimu za Wizara ya Maji zinaonesha hadi Aprili, 2024 Mtandao wa Majitaka umefikia kilometa 1455.93 ikilinganishwa na kilometa 1416.9 za Aprili, 2023.

Anasema maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao wa majitaka na uondoaji wa majitaka kwa magari ambayo hupeleka kwenye miundombinu ya kutibu majitaka, serikali itaendelea kuwekeza zaidi katika usafi wa mazingira ili kufikia malengo iliyojiwekea.

"Yatupasa kufahamu kuwa ajenda ya usafi wa mazingira ni mtambuka na ndio maana hata sera zetu za afya, maji na mazingira zote zinaongelea suala hili la usafi wa mazingira, nina Imani kongamano hili litaitendea haki ajenda ya usafi wa mazingira kwa kuja na mawazo chanya yenye lengo la kuboresha usafi wa mazingira nchini ili kuchochea maendeleo ya watu,"anasema.

Naye Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, anaipongeza EWURA kwa kuandaa kongamano hilo ambalo limewakutanisha wadau mbalimbali kujadili namna ya kuimarisha masuala ya usimamizi wa mazingira katika miji.

Aidha, anasema kuzinduliwa kwa mwongozo huo kutasaidia mamlaka za maji na wadau mbalimbali katika usimamizi wa huduma za usafi wa mazingira na tope kinyesi.

Anazikumbusha Mamlaka za Maji nchini kuzingatia mwongozo huo ambao unaweka misingi, mipaka na wajibu na majukumu ya utoaji huduma za usimamizi wa tope kinyesi zinazofanywa na mamlaka hizo.

"Ni vyema mnyororo wa huduma za usafi wa mazingira kuanzia kukusanya, usafirishaji na matumizi ya tope kinyesi ukazingatiwa ili kulinda afya za wananchi, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan tutahakikisha malengo ya utoaji huduma za usafi wa mazingira yanafikiwa,"anasema.

# SERIKALI KATIKA OPERESHENI KUFIKIA MAPINDUZI YA UZALISHAJI SAMAKI, KUANZIA VIFARANGA WAKE

Inatoka Uk 12

kuchakata mazao ya uvuvi unaendelea Kilwa," anasema Lyobah.

**CHANGAMOTO**

Lyobah anasema kwamba uvuvi wa sasa zaidi hauna tija kwa sababu vyombo vinavyotumika vina uwezo mdogo, jambo linalosababisha wavuvi kutofikia uvuvi mkubwa yaani bahari kuu.

"Bahari imegawanyika kwa maeneo kama manne ambayo ya ndani na EEZ. Ndani tunaita ni maji ya kitaifa (territorial water), haya m,wenye nchi una mamlaka ya kuyasimamia. Baada ya maili 12 ni eneo la kiuchumi la bahari 'EEZ' ni maji unayoruhusiwa kuyatumia na nchi husika na anayehitaji ataomba kibali.

Pia kuna maji ya kimataifa na kila mtu anaweza kutumia ila inatakiwa ujitambulishe kwa kupepea kwa bendera ya nchi yako. TAFICO tumerudi kivingine kwa kutumia uvuvi wa kisasa ili kwenda mbali zaidi na si katika maji ya ndani ambayo unaweza kuleta mgogoro na wavuvi wadogo.

Tutawekeza katika ufugaji wa samaki na pia kwenye uvuvi mkubwa wa kibiashara," anaeleza.

Tulikuwa na meli ya urefu wa mita 22 tulikuwa tunavua mwanzoni mwa eneo la EEZ (exclusive economic zone) karibu na bahari kuu. Tunalenga kuvuka eneo la EEZ ni eneo la nchi nyingine ambako unafuatwa tu utaratibu na unaendelea kuvua.

Lengo kuu ni samaki aina jodari ambaye tabia yake ni kuhama, leo yupo bahari inayomilikiwa na nchi hii kesho karudi Tanzania, au Ushelisheli!" anaeleza Lyobah.



# Serikali yataka mashirika kuwekeza bima ya afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeyataka mashirika yasiyo ya kiserikai yanayojihusisha na utoaji wa huduma katika sekta ya afya nchini kuwekeza nguvu kwenye bima ya afya kwa wote na uboreshaji wa huduma za afya.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel wakati akifungua kikao kati ya serikali na mashirika hayo jijini hapa.

Dk.Mollel, alisema kwa sasa vipaumbele vya serikali katika sekta ya afya ni bima ya afya kwa wote na uboreshaji wa huduma za afya nchini kuanzia ngazi ya zahanati.

"Moja ya kazi yenu ni kushirikiana na serikali kutekeleza vipaumbele vyake, hivyo basi kwa sasa vipaumbele vya serikali ni suala la bima ya afya kwa wote pamoja na kuboresha huduma za afya nchini.

"Hivyo basi mnapaswa kuwekeza nguvu zote pamoja na rasirimali zenu ili kuunga mkono ajenda hii," alisisitiza Dk. Mollel

Alisema katika kipindi cha uongozi wa serikali iliyoko madarakani, uwekezaji mkubwa umefanyika katika sekta ya afya, hivyo wadau hao hawanabudi kuunga mkono jitihada hizo.

"Kama tatizo la kansa (saratani) kipindi cha nyuma nchini wagonjwa wengi walikuwa wakienda pale Ocean Road, wakiwa katika hatua za kufa, lakini kwa sasa kutokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali zaidi ya asilimia 70 ya wagonjwa wanakwenda wakiwa bado kansa yao inaweza kutibika. "Hii inamaanisha uwekezaji uliofanywa na serikali ya awamu ya sita chini ya mama yetu, Rais Samia Suluhu Hassan, wagonjwa wanagundulika mapema kabla hali haijawa mbaya hivyo wengi wanapata tiba na kupona,"alisema Dk. Mollel

> **"Moja ya kazi yenu ni kushirikiana na serikali kutekeleza vipaumbele vyake, hivyo basi kwa sasa vipaumbele vya serikali ni suala la bima ya afya kwa wote ...**

Alisema katika kipindi cha miaka 60 iliyopita ni hospitali mbili tu ambazo zilikuwa na kipimo cha CT Scan, kwa sasa kutokana uwekezaji uliofanya, kipimo hicho kipo katika maeneo mengi ya nchi. Akizungumzia kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa M POX, Dk. Mollel, aliwataka wananchi kuendelea kuwa watulivu na kuacha kuendeshwa kwa matukio.

Mwenyekiti wa mashirika hayo, Dickens Mbwana, alisema lengo la kikao hicho ni kuandaa mipango ya utekelezaji kulingana na vipaumbele vya serikali.

"Tunaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika sekta ya afya, ombi letu ni kuendelea kushirikishwa na serikali katika vipaumbele vyake na utekelezaji wa afua ikiwemo mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema Mbwana



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata (wa tatu kushoto), akiwanawisha maji baadhi ya viongozi wa dini kwa kutumia vitakasa mikono, baada ya kumaliza kikao cha wadau wa afya wa mkoa huo juzi, ikiwa ni sehemu ya tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa homa ya nyani (M-POX). **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Tahadhari homa ya nyani yatolewa kwa wakazi Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKAZI mkoani hapa wametakiwa kuchukua tahadhari kwa kujikinga na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Homa ya Nyani (M-Pox).

Mkuu wa Mkoa Singida, Halima Dendego, alitoa rai hiyo katika mkutano wa wadau wa afya.

Dendego, aliwataka wakazi hao kuzingatia njia mbalimbali za kujikinga na ugonjwa huo, ikiwamo kutumia vitakasa mikono.

Alifafanua kuwa ametoa tahadhari hiyo kutokana na ugonjwa huo hauna tiba ya moja kwa moja na bado haujasambaa wala kuingia nchini.

Alisema jitihada kubwa zinapaswa kuelekezwa katika kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huo.

Dendego, alisema serikali ya mkoa huo imeweka mikakati kukabiliana na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuwafikia wananchi wengi kwa wakati mmoja kupitia utoaji wa elimu kwa umma.

Alisisitiza kuwa njia kama vipindi vya redio na televisheni na mafunzo ya moja kwa moja katika maeneo ya makazi na biashara ni muhimu katika kuhakikisha ujumbe unawafikia watu wengi kwa wakati mmoja.

"Tuwekeze nguvu kubwa katika kujikinga na ugonjwa huu, tuwafikie watu wengi kwa wakati mmoja kwa kutumia redio na mafunzo juu ya ugonjwa huu yatolewe katika shule, masoko, standi, maeneo ya kuabudu, pamoja na mikosanyiko," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Alisema mafunzo hayo yanapaswa kuwa ya kina na kueleweka ili jamii iweze kuchukua tahadhari kujikinga na kuzuia maambukizi mapya.

Katibu Tawala Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, ameagiza vifaa vilivyokuwa vinatumika kunawia mikono wakati wa Covid-19, vifanye kazi hiyo ili kuwalinda wakazi hao na ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Victorina Ludovick, alisema wanaendelea kuchukua tahadhari na kupanga mikakati kuzuia ugonjwa huo.

Alisema kila mkazi anapaswa kufuata kanuni za afya na maelekezo ili kujizuia yeye, familia yake na watu wanaomzunguka na Mpox.

Ugonjwa huo huambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, pia unaambukiza kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine kupitia kugusana na mtu aliyeambukizwa au vifaa vilivyotumiwa na mgonjwa kwani maji maji ya mwili au vidonda vya mtu aliyeathirika hubeba vimelea vya Mpox.

# Wajumbe NACoNGo, wasajili wapigwa msasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAJUMBE wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACoNGO) na Wasajili Wasaidizi wametakiwa kusimamia uratibu, usajili na ufuatiliaji wa shughuli zao katika mamlaka za mikoa na serikali za mitaa ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuzingatia mila na desturi za Mtanzania.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Felister Mdemu alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua mafunzo kwa wajumbe hao jijini hapa.

Felister, alisema kanzi data inaonesha mashirika 9,776 yanafanya kazi kwenye sekta mbalimbali na ili kurahisisha uratibu, baraza hilo na wasajili hao ni vyombo muhimu kuratibu usajili na kufuatilia shughuli zinazofanywa kwenye mamlaka hizo za mikoa na serikali za mitaa.

"Baada ya mafunzo haya tunategemea kutakuwa na ongezeko la mashirika kufuata sheria na kanuni hasa utumaji wa taarifa za utekelezaji na ulipaji wa ada,"alisema.

Alisema wizara inatambua kuna changamoto katika uratibu kama vile ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya mashirika, mafunzo ya mfumo wa Kieletroniki wa usajili na uratibu (NIS) na ufinyu wa bajeti ya kufanya ufuatiliaji wa shughuli zao.

"Wizara imeamua kuandaa mafunzo haya ili kuwapitisha katika sheria, kanuni na miongozo, mfumo wa kieletroniki wa usajili na uratibu (NIS) maana umefanyiwa mabadiliko hasa baada ya kuongezewa kipengele cha ramani ya kidigitali,"alisema.

Vilevile, alisema wizara hiyo itahakikisha miradi inayotekelezwa na mashirika hayo inanufaisha jamii ili kuleta maendeleo nchini. Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika hayo, Mwantumu Mahiza, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa washiriki hao kwa sababu wanafanya kazi kwa karibu na mashirika hayo ambao ni wadau muhimu wa maendeleo nchini.

# Wahamasishwa kujiandikisha, kushiriki uchaguzi S/Mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Asia Messos amewataka wakazi wa kata za Nkalakala na Miganga kujitokeza kwa wingi kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika nchini Novemba 27, 2024.

Messos, alitoa wito huo juzi wakati wa ziara yake ya kikazi ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wakazi wa kata hizo zilizopo wilayani hapa.

"Mwaka huu tutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tujitokeze kwa wingi wetu tushiriki uchaguzi huu kwa maendeleo ya kata zetu, usikubali mtu mwingine akuchagulie kiongozi wakati una uwezo wa kupiga kura," alisema.

Alisema ili mwananchi aweze kupiga kura siku hiyo, anapaswa kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapiga kura ambalo uandikishaji wake utafanyika kuanzia Oktoba 11 hadi 20, 2024 wilayani hapa.

Aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi kushiriki uchaguzi huo kwa kuwania nafasi za uongozi na kushiriki maamuzi yatakayoleta maendeleo ndani ya kata zao.

"Kina mama tujitokeze kwa wingi kuchukua fomu tuwe na viongozi wanawake kwenye nafasi za maamuzi," alisema.

Akizungumzia kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, alisema kwa Mkoa wa Singida unatarajia kufanyika Septemba 25, mwaka huu na kuwataka wananchi kujitokeza kuhuisha taarifa zao na ambao hawana kadi kujisajiri ili wapate kadi ya mpiga kura

Awali akieleza mambo makubwa yaliyofanywa na serikali ya awamu ya sita katika miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Messos alisema halmashauri hiyo imepokea zaidi ya Sh.Bilioni 60 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu, afya, michezo na kilimo.





# Ofisa mtendaji chupuchupu jela kwa ubadhirifu

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya imemtoza Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kisyosyo, Anania Mwalukanga faini ya Sh. 500,000 na kunusurika kufungwa jela miaka miwili baada ya kupatikana na hatia ya ubadhirifu wa mali ya umma.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Wilaya ya Kyela, Paul Mabula baada ya ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka mahakamani hapo kuthibitisha bila kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, mshtakiwa huyo alikusanya fedha za halmashauri ya wilaya hiyo ya Kyela, zaidi ya Sh. Milioni 1.8 na kutumia kwa matumizi yake binafsi.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Sospeter Tyeah, alidai kosa hilo ni kinyume cha Sheria kifungu namba 28(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329.

"Ofisa huyu alikuwa na jukumu la kukusanya fedha za serikali ambazo ni ushuru pamoja na mapato mengine na baada ya kukusanya hakuwasilisha halmashauri jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa," alidai Tyeah.

**"Ofisa huyu alikuwa na jukumu la kukusanya fedha za serikali ambazo ni ushuru pamoja na mapato mengine na baada ya kukusanya hakuwasilisha halmashauri jambo ambalo ni..."**

Baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka, Hakimu Mabula, alisema umedhihirisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Mabula, alisema mahakama hiyo ina muhukumu kulipa kiasi hicho cha fedha, kulipa faini au kutumikia kifungo cha miaka miwili jela kwa kosa la ubadhirifu wa mali ya umma.

Baada ya mshtakiwa huyo kurejesha fedha hizo, kulipa faini, hakimu huyo aliamuru aachiwe huru huku mahakama hiyo ikimpa onyo la kutorudia kutenda kosa kama hilo.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Cuthbert Mwinuka (wa tano kushoto), akiwasaidia vijana kupakia mchanga kwenye mashine ya kusaga mawe katika moja ya migodi ya dhahabu katika Kijiji cha Itumbi, Kata ya Matundasi, wilayani humo juzi, alipofanya ziara ya kuwatembelea wachimbaji wadogo na kusikiliza kero zao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM 'hapatoshi', yawabana viongozi wa serikali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe kimewaagiza wakuu wa taasisi za serikali mkoani hapa kukamilisha ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa wakati ili kuondoa kero sugu kwa wananchi.

Agizo hilo lilitolewa juzi kwenye kikao cha majumuisho ya mambo yaliyojadiliwa ndani ya Mkutano wa Halmashauri Mkuu ya CCM Mkoa wa Njombe na Katibu wa Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa chama hicho wa mkoa huo, Josaya Luoga.

Luoga, alisema chama hicho hakitaki kusikia kero na malalamiko ya wananchi yakiendelea ya kukwama kwa miradi hiyo ambayo serikali inapeleka fedha mara kwa mara.

"Kama kuna viporo vya kazi za miradi ambayo inafanywa kwenye mkoa wetu wa Njombe zihakikishwe zinatatuliwa na zile kero ambazo zipo ndani ya uwezo wao viongozi wa serikali wazitatue kwa sababu hawategemei kupata maswali mengi kutoka kwa wananchi," alisema.

Alisema wameelekeza viongozi wa serikali watoe taarifa sahihi kwa wananchi juu ya uwepo wa maboresho ya daftari la mpiga kura kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024.

Katibu wa CCM wa mkoa huo, Julius Peter, alisema lengo la kikao hicho ni kuendelea kuboresha mahusiano kati ya chama hicho na serikali ya kuhudumia wananchi.

Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Deo Sanga, alisema viongozi wa chama hicho na serikali wanapaswa kwenda kuwaambia wananchi Rais Samia Suluhu Hassan amepeleka fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo mkoani hapa.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Judica Omary, alisema kwa kipindi cha miaka mitatu, serikali imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwemo maji, umeme na barabara.

Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Wilson Joel, akizungumzia kuhusu mchakato wa upatikanaji wa pembejeo za ruzuku za kilimo katika msimu mpya wa kilimo mwaka 2024/2025, alisema kila halmashauri itakuwa na vituo vitatu vya mawakala wakubwa kwa ajili ya kupata pembejeo hizo.

# Halmashauri, sekta binafsi zatakiwa kushirikiana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI nchini zimetakiwa kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuboresha maisha ya wananchi.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP), Frola Tenga alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati wa mafunzo kwa watendaji wa serikali wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu manunuzi wa umma, sheria ya PPP na matumizi ya takwimu.

Alizitaka halmashauri zote kuwasilisha kwa wataalamu wa ubia mawazo ya miradi ya maendeleo iliyopo maeneo yao ambayo itaingizwa kwenye ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

Aliwataka maofisa ugavi, manunuzi, maofisa mipango wa halmashauri kuibua miradi ili serikali itekeleza kupitia ubia na sekta hiyo.

"Kama halmashauri itabaini haina uwezo wa kutafuta wawekezaji, basi sisi PPP tutasaidia kuwapata, mkiona fursa ama wazo lolote ambalo mnadhani linaweza kuingia kwenye miradi ya ubia na sekta binafsi iwasilisheni kwetu, sisi tutawasaidia," alisema Frola.

Alitaja maeneo ambayo serikali inaweza kutekeleza kupitia ubia na sekta hiyo binafsi kuwa ni pamoja na uboreshaji na ukarabati wa miundombinu, ujenzi na uendeshaji wa miradi.

Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) wa Kanda hiyo, Paschal Manono, alisema fursa zilizopo katika sheria ya ununuzi wa umma namba 10 ya mwaka 2023 ni kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika ununuzi.

Mnono, alisema lengo la sheria hiyo ni kutekeleza miradi kwa thamani halisi ya miradi husika na kudhibiti ubadhirifu kwa manufaa ya wananchi.

Alisema malengo mengine ya kutunga sheria hiyo ni kutumia bidhaa za ndani kukuza kipato kwa wananchi wanaojishughulisha na uzalishaji .

Alionya kuwa ni kosa la jinai kwa mtumishi kufanya ununuzi wa umma nje ya mfumo wa kielektroniki.

Aliwataka maofisa ugavi na ununuzi kuzingatia mfumo huo ili kuepuka matatizo yanayoweza kuwakumba.

Mtakwimu Mwandamizi Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Boniface Simpoli, alisema matumizi ya takwimu sahihi kwenye ununuzi wa umma na miradi ya PPP zitasaidia kupanga na kufanya uwekezaji.

Simpoli, alisema miradi inapotekelezwa itakuwa inazingatiwa idadi ya wananchi watakaonufaika na shughuli zao za kiuchumi katika eneo husika la mradi.

Alisema kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi wa umma, kinatambua makundi maalumu, hivyo matumizi sahihi ya takwimu yatasaidia kuwatambua, kuhudumiwa na namna ya kuyashirikisha kwenye ununuzi.

Akifungua mkutano huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Lodrick Mpogolo, aliwataka watendaji kuzingatia mafunzo yaliyotolewa na wataalamu kutekeleza majukumu yao bila ya kukinzana na sheria zilizowekwa.

Mpogolo, aliwahimiza kutumia mafunzo hayo maeneo yao kwa ajili ya kuboresha ufanisi na utendaji wa shughuli za Serikali.





# Mbunge aeleza sifa kuu tatu za Juma Duni Haji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MBUNGE wa Mji Mkongwe, Ali Saleh, amesema aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji ni mpenda haki, mkweli, asiye na kinyongo.

Alisema hayo juzi Zanzibar wakati akisoma wasifu wa mwanasiasa huyo mkongwe katika sherehe za kumpongeza kutokana na utumishi wake uliotukuka katika chama hicho.

Alisema Juma Duni ni mtu mwenye uwezo wa kujenga hoja, kushawishi na hata kushawishi watu, kuzungumza na kila rika.

“Muda wote, hata wakati ambapo hakueleweka, alibaki katika msimamo wake na hakuhitaji kujitetea bali alijaribu kujenga hoja ili aeleweke,” alisema.

Akitolea mfano, Saleh alisema kuna wakati Juma Duni alipata msukosuko akiwa serikali kwa kuamuru mchele upelekwe Pemba kwa kuwa kulikuwa na uhaba uliosababisha kuwapo na njaa na bahati mbaya jahazi moja kupotea.

Alisema licha ya msukosuko huo lakini alichowaambia wakubwa wake ni kuwa alilazimika kufanya hivyo ili kufanikisha mambo mawili likiwamo kuwaokoa wakazi wa Pemba na njaa kwa vile usafiri wa meli za serikali ulikuwa na ugumu, lakini pili kuiepusha serikali na lawama hasa ya kisiasa.

> **“Muda wote, hata wakati ambapo hakueleweka, alibaki katika msimamo wake na hakuhitaji kujitetea bali alijaribu kujenga hoja ili aeleweke,” alisema.**

Akieleza wasifu huo, alisema maamuzi mengine makubwa aliyoyafanya alipokuwa sekta ya biashara miaka hiyo ni pale alipomkabili Waziri Kiongozi Maalim Seif Sharif Hamad na kumpa fikra kuwa wakati umefika kwa serikali kuruhusu wafanyabiashara na watu wenye fedha waruhusiwe kuleta bidhaa na vyakula.

Alisema mwanasiasa huyo pia alikuwa mwalimu wa shule katika masomo ya sayansi na katika watu maarufu aliowafundisha ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan Rais, Haroun Ali Suleiman Waziri wa Katiba na Sheria, Ismail Jussa Makamo Mwenyekiti wa ACT- na Dk. Naufal Kassim.

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, alisema unapopigania uadilifu na haki katika nchi huwezi kuchoka iwapo jukumu hilo halijakamilika na anayechoka huwa hana tabia ya uongozi.

Alisema Juma Duni amewafunza watu na viongozi wengi kuwa kiongozi bora ambaye hakujenga uzio katika uongozi wake, bali aliwafunza watu masuala mbalimbali.

Kiongozi wa chama hicho, Doroth Semu, alisema chama hicho kimefanya utafiti juu ya namna bora ya kuwaenzi viongozi na kwamba kimeanzisha sera rasmi ya kuhakikisha wanatimiza jukumu hilo.

Alisema chama hicho kitaendelea kuwaenzi kwa vitendo siyo tu viongozi wa ngazi ya juu waliostaafu, lakini hata watumishi wa kawaida kwa kupatiwa huduma na stahiki mbalimbali ikiwamo makazi kwa wale wasiokuwa nayo.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Ismail Jussa Ladhu, alisema Juma Duni amepata bahati ya heshima kubwa




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza wakati akifungua kongamano la saba la Uongozi la Wanawake Wahasibu Tanzania, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: OMPR**

# Wahasibu wanawake watakiwa kuleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu**

WAHASIBU wanawake wametakiwa kuweka mikakati imara na thabiti ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii na taifa, ili kutanua wigo wa kuhamasisha usawa na haki kwa wanawake na wasichana.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa wito huo wakati akifungua Kongamano la Saba la Uongozi la Wanawake Wahasibu Tanzania, akimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema wahasibu wanawake wana fursa ya kujenga mtandao imara wa kusaidiana na kuhamasishana kufikia maendeleo waliokusudia hasa katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Alisema serikali itaendelea kuwa washirika wa kimkakati na kusimama pamoja na TAWCA katika kuboresha mazingira ya kazi, kuwekeza katika elimu, fursa sawa za maendeleo pamoja na kuondoa vikwazo dhidi ya wanawake.

Alisema TAWCA imekuwa mstari wa mbele katika kuwainua wajasiriamali kwa kuwapa taaluma za kifedha na stadi za maisha ili kuyafikia malengo waliojiwekea katika biashara zao.

Hivyo, alikipongeza Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania kwa shughuli wanazozifanya ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake, kuwasaidia wahasibu wachanga kufanya vizuri katika fani zao kwa kuwakumbusha kuzingatia maadili ya kazi zao.

Pia, alitoa wito kwa wadau kuunga mkono juhudi za serikali kusaidia upatikanaji wa kundi bora la wanawake lenye kujitegemea katika kuboresha na kuinua uchumi katika jamii na taifa.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Juma Makungu Juma, alisema serikali inatambua mchango wa wanawake wahasibu nchini katika kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na uaminifu mkubwa.

Alisema serikali itaendelea kufanya kazi kwa karibu na TAWCA ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa chama hicho.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la TAWCA, Neema Kiure, alisema lengo la kongamano hilo ni kuwajengea uwezo na kupeana taaluma na ujuzi kwa wahasibu wanawake, ili kuchochea mabadiliko ya kiutendaji na kimaendeleo katika kada ya uhasibu nchini.

Alisema TAWCA imekuwa ikitoa elimu kwa wajasiriamali wanawake juu ya kutunza kumbukumbu za biashara na namna ya matumizi mazuri ya mikopo wanayopatiwa ili waweze kupata matokeo yenye tija na faida zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Taifa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), Pius Maneno, alisema taaluma ya uhasibu inakuwa kwa kasi nchini, kwamba hadi kufikia mwaka 2024 wahasibu wanawake waliosajiliwa wamefikia asilimia 34.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na TAWCA ni kudhibiti na kusimamia taaluma ya uhasibu kwa kuwapatia ujuzi na nyenzo wahasibu wanawake.

## Serikali kutupia jicho zaidi sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali inaendelea kutoa kipaumbele sekta ya afya kutokana na kuwapo changamoto nyingi za kiafya ikiwamo ongezeko la magonjwa ya moyo kwa watoto.

Aliyasema hayo juzi ofisini kwake Migombani Zanzibar, alipokutana na wataalamu wa tiba ya maradhi ya moyo kutoka Shirika la Kimataifa la Marekani la Global Cardiac Allience.

Shirika hilo linajishughulisha na utoaji wa tiba, upasuaji wa moyo kwa watoto pamoja na utoaji wa mafunzo kwa madaktari wa moyo sehemu mbalimbali duniani.

Othman alisema kutokana na hali hiyo serikali inalazimika kila mwaka kutumia gharama kubwa kwa tiba ya moyo kwa watoto hasa nje ya nchi, jambo ambalo ni changamoto kubwa kwa nchi.

Alisema kunahitajika wadau kuunga mkono juhudi hizo kwa kuanzisha kituo cha tiba hiyo, ili kusaidia uimarishaji wa afya kwa jamii Zanzibar.

Alisema kwamba kuwapo wadau watakaosaidia kupambana na suala la maradhi hayo kutasaidia kupunguza na kutoa ahuweni ya gharama za matibabu hayo kwa serikali na jamii visiwani humo.

Hivyo, alisema kwamba kutokana na hali hiyo serikali ipo tayari kushirikiana na wadau na uwekezaji katika kusaidia ufumbuzi wa changamoto ya maradhi ya aina hiyo ambayo yanagharama kubwa katika matibabu yake nje ya nchi.

Alisema serikali inafurahishwa na inahitaji kuwapo kituo cha tiba ya moyo na pia kutolewa mafunzo na kujengewa uwezo madaktari wazalendo ambao ni muhimu katika kusaidia na kupunguza changamoto za maradhi yakiwamo ya moyo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazuri, alisema suala la matatizo ya moyo kwa watoto linaendelea kuwa changamoto kubwa na kwamba zaidi ya watoto 600 hukumbwa na tatizo hilo kila mwaka nchini.

Alisema kutokana na hali hiyo bado suala hilo linaendelea kuwa changamoto kubwa kwa Zanzibar na kwamba serikali inalazimika kuwapeleka watoto kupatiwa matibabu ya moyo nje ya nchi ikiwamo Israel na India.

Mtaalamu aliyeongoza ujumbe huo kutoka Shirika la Global Cardiac Allience la Marekani, Profesa William Novick, alisema shirika hilo linaendelea kusaidia matibabu hayo kwa njia mbali mbali ikiwamo upasuaji, utoaji wa mafunzo kwa madaktari wazalendo.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHACHA KITEGE ELISHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2687/0121 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **RUBANA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2021**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MAR/BUN/6242/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZAINABU BILALI ABDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1118-0028 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MLONGWEMA SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/189135/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 9789 YA MWAKA 2024**
**ZUWENA SHABANI MALAMULA .........MDAI**
**DHIDI YA**
**FATMA MKUKI...............1. MDAIWA**
**NELUKA SECONDARY SCHOOL ..............2. MDAIWA**
**MULDALIFA SECONDARY ...............3. MDAIWA**
**TANZANIA EDUCATION SUPORTING AGENCY......4. MDAIWA**

**KWA: FATMA MKUKI**
**MULDALIFA SECONDARY**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
**K**wa kuwa Mdai aliyetajwa hapo juu amefungua shauri la Madai dhidi yako, Maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinazopatikana katika Mahakama hii, hivyo basi, unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 11/09/2024 saa Moja na nusu (07:30) asubuhi mbele ya Mhe. E.Y. Mkwizu, J. Kujibu madai hayo dhidi yako, Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambayo unatarajia kuvituma katika utetezi wako siku hiyo,

**ANGALIA:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 27 Mezi Mei 2024

NAIBU MSAJILI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 297 LA 2024**

**RAMADHANI TARATIBU ABDALLAH NA WENZAKE 5......... MUOMBAJI/WAOMBAJI**


**DHIDI YA**

- **AGNELA JUSTINE MAGENZI 6.MACHARRI SAMWEL**
- **SAMWEL YOBU MEENA**
  **7.ADVENT JONATHAN**
- **CHEMWEMWE PATRIC**
  **8. TRIFEENA KHAMIS**
- **MAGRETH JUSTIN**
  **9. KBM-SONS & COMPANY LTD**
- **SHEDRACK DANIEL**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**RAMADHANI TARATIBU ABDALLAH** amefungua /wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni( Mwananyamala) shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 23/10/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 Mwezi 09 ,2024

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOSEPH WENCESLAUS KANJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **No. S0341-0335** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SANGU SECONDARY SCHOOL mwaka 2012**, Cheti cha kidato cha sita chenye No. S1043-0624 Kilchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TUKUYU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Vyeti hivi vimepotea Jijini **DAR ES SALAAM.** Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/39513/2024.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI SUB- REGISTRY**
**AT MOSHI**
**MISC.CIVIL APPLICATION NO.39 OF 2023**
**(C/F Talaka 14/2020,Moshi Urban Primary court and Matrimonial Appeal No. 06/2020)**

**SAIDA RAJABU CHADUA.....................APPLICANT**
**VERSUS**
**CHARLES JACOBO NDAGULA..................RESPONDENT**

**TO CHARLES JACOB NDAGULA**

**NOTICE FOR RULING,**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for Ruling in the High Court of Tanzania at Moshi on 25 day of th September ,2024 at 09:00 a.m. before Honourable L.M. MONGELLA ,Judge.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the NIPASHE.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
GIVEN UNDER my hand and seal of the Court this 29th day of August ,2024.

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LADISLAUS EDWARD MUSHI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili

**MC 503 AVQ**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**TAARIFA YA POLISI:**

**PHQ/ARU/ARU/32769/2024.**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5566 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PONTIUM MUTA MUTASHUBIRWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DEOGRATIAS PROTAS BABIRIGI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 08 day of 10, 2024.
**Dated at DAR ES SALAAM this 09 day of 08, 2024.**

Senior Resident Magistrate

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SAONGEA**

**MAOMBI NAMBA 113/2023**

**NIKODEM VITALIS MWENDA ———————MUOMBAJI .**
**DHIDI YA**
**LUKAS LUKAS NDOMBA**
**MARIA SIKUMOJA NGINDO**
**NICODEM NICODEM MWENDA ————————-WAJIBU MAOMBI.**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi wa pili na watatu ,mnataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu .Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au Wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 09/09/2024 saa 5:00 asubuhi.Shauri linakuja kwa ajali ya kusomwa Hukumu.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusoma Hukumu bila kujali uwepo wenu.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 16/08/2024.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**RUVUMA**

## KUPOTEA KWA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

**THERESIA SHIJA MAKONO**

anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 55 kitalu "VV" Ngokolo Manispaa ya Shinyanga kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

Taarifa ya polisi

**PHQ/SHI/SHI/7994/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**YORKE L. MWAMAPANDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S 1349/0065** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYAKAHURA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/190343/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 19814 of 2024**
**In the matter of the estate of the late CHRISTOPHER JAPHET KAZERI**
**And**
**In the matter of application for Letters of administration by SECILIA JOHN DOMINICK AND JAPHETI WAZERE PHINIAS**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 10 ...................... 2024
Dated at Dodoma this 05 day of 09................2024

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 20389 OF 2024**
**In the Matter of the late SALOME LEOPOLD MOSES**
**And**
**In the Matter on an Application for letters of administration by GLORY GEOFREY JUSTINE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 17th day of 09.........2024
Presented for filling this 28 Day of August.........2024

........................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 20388 OF 2024**
**In the Matter of the late LEOPOLD MOSES DISSI**
**And**
**In the Matter on an Application for letters of administration by GLORY GEOFREY JUSTINE**

**GENERAL CITATION**
**Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30th Day of SEPTEMBER............2024
Presented for filling this 28TH Day of August.......2024

........................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MBEYA**
**KITUO CHA IYUNGA MKOA WA MBEYA**
**SHAURI LA MADAI/NDOA Na......29/2024**

**JINA LA MDAI: CATHERINE GUSTAVU**
**JINA LA MDAIWA:EMMANUEL DAVID**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA:EMMANUEL DAVID**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta Madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai:**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 6 Mwezi 9 Mwaka 2024 saa2:30 Asubuhi/Mchana kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 8 Mwaka 2024

..............................................
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO IYUNGA-MBEYA**


## KUPOTEA KWA CHETI



**STEPHANO MAKOYE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2808-0137 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KISHAMAPANDA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MAR/BUN/6442/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAPPINESS JEREMIA MAHONA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0612-0040 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KAGANGO SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MOR/MAL/29650/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...32/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAJABU JUMA NIA wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LUO RAJABU NIA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 09 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 05 mwezi 09 mwaka 2024

..............................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID DENSON HINJO**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA RAV 4, RANGI NYEUSI YENYE USAJILI T895DHX CHASISI NAMBA ZCA260048416. KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/13542/2024.**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.21282 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late SELVASIUS TOTNANT MWAGENI**
**And**
**In the matter of Application for letters of administration by HAIKA TUMAINI MNDEME**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 day of 10, 2024
Dated at DAR ES SALAAM this 03 day of 09, 2024

Principal Resident Magistrate

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yaituhumu Russia kuingilia uchaguzi mkuu

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imeituhumu Russia kufanya kampeni ya kuingilia uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Katika kulipiza kisasi Marekani imewashtaki na kuwawekea vikwazo watangazaji na wasimamizi wa vyombo vya habari vya serikali ya Russia kutokana na kuhusika na kampeni hiyo.

Wizara ya sheria, serikali na hazina ya Marekani, ilitangaza hatua zilizochukuliwa Jumatano katika kukabiliana vikali na shughuli zinazodaiwa kuingilia uchaguzi huo.

Mwanasheria Mkuu wa serikali, Merrick Garland alilishutumu shirika la utangazaji la RT, linalomilikiwa na serikali ya Russia kwa kuilipa kampuni ya Tennessee dola milioni 10 ili kuunda na kusambaza maudhui kwa watazamaji wa Marekani wenye ujumbe fiche wa serikali ya Russia.

Mkuu wa RT Margarita Simonyan alikuwa mmoja wa watu 10 walioidhinishwa kuwekewa vikwazo kwa madai ya kujaribu kuharibu imani Wamarekani.

RT imekanusha kuhusika na tuhuma hizo.

Hata hivyo, Garland alisema kuwa Russia ilitaka kupata matokeo katika kinyang'anyiro cha nafasi ya urais kati ya Donald Trump na Kamala Harris.

Msemaji wa usalama wa taifa wa Ikulu ya Marekani, John Kirby, alisema kuwa mpango huo wa unalenga kupunguza uungwaji mkono wa kimataifa kwa Ukraine na kuimarisha sera na maslahi yanayoiunga mkono Urusi.

Alisema mpango huo pia inaathiri wapiga kura wa Marekani.

Afisa wa Hazina alisema kuwa RT na vyombo vingine vya habari vya serikali ya Russia vilijihusisha na kampeni mbaya ya kuajiri kwa siri washawishi wa Marekani bila kujua ili kuunga mkono shughuli zao. ***BBC.***




Wananchi nchini Kenya wakiandamana kupinga kuongezeka kwa visa vya mauaji ya wanawake na unyanyasaji jijini Nairobi jana. **PICHA: BBC**

# Uingereza yazuia silaha kwa Israel

**LONDON, Uingereza**

Uingereza imeeleza uamuzi wake wa kusitisha baadhi ya mauzo ya silaha kwa Israel, inalenga kutotumika katika mashambulizi katika Ukanda ya Gaza ambayo yanakiuka haki za kibinadamu.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema uamuzi huo kuwa wa ni kitendo cha aibu.

Netanyahu alisema kupitia ukurasa wake wa kijamii kwamba uamuzi huo utawapa ujasiri wanamgambo wa Hamas.

Siku ya Jumatatu, Uingereza ilisitisha leseni zipatazo 30 kati ya 350 za kuuza silaha kwa Israel.

Waziri wa Ulinzi wa Uingereza, John Healey alisisitiza kuwa Uingereza itasalia kuwa mshirika mkuu wa Israel, na kwamba usalama wake hautayumbishwa na uamuzi huo.

Mawaziri wa serikali ya nchi hiyo walisema silaha hizo zinaweza kutumika Ukanda wa Gaza na kukiuka sheria za kimataifa.

Balozi wa Palestina nchini Uingereza, Husam Zomlot, alielezea marufuku hiyo ya sehemu ya silaha kama hatua muhimu ya kwanza kufanywa na Uingereza kutimiza majukumu yake ya kisheria chini ya sheria za nchi hiyo na kimataifa.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International ya Uingereza ilisema hatua hizo ni ndogo kulingana na mashaka yanayotokea Gaza.

Hata hivyo, wengine waliukosoa muda wa kutangazwa kwa mpango huo, ambao uliambatana na siku ya mazishi ya mateka sita waliouawa huko Gaza wiki iliyopita.

"Ilikuwa uchungu sana kuona nyuso za mateka waliokufa," Healy aliiambia BBC, lakini aliongeza kuwa muda wa uamuzi huo ni kama msukumo kwani mchakato huo wa kisheria na kupitishwa na bunge.

Wakati huo huo, Waziri mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisisitiza tena kwamba majeshi ya Israel hayataondoka kwenye Ukanda wa Philadelphi, akisema ni muhimu kwa kimkakati katika eneo la kusini mwa Gaza kwenye mpaka na Misri.

Aliviambia vyombo vya habari vya kigeni mjini Jerusalem kwamba yuko wazi kufikiria njia mbadala za kuwepo kwa wanajeshi wa Israel kwenye mpaka wa Gaza na Misri, kama sehemu ya makubaliano yoyote ya siku za usoni ya kusitisha mapigano, lakini hakuona hilo likifanyika.

Netanyahu alidai kwamba wanajeshi wa Israel lazima wabaki ili kuzuia silaha na ikiwezekana mateka wa Israel kupitishwa kinyemela kuvuka mpaka.

Hamas ilisema katika taarifa iliyonukuliwa na shirika la habari la Reuters kwamba uamuzi wa Netanyahu kutojiondoa katika ukanda wa Philadelphi ni jaribio la kukwamisha makubaliano ya kusitisha mapigano, na kuongeza kuwa ni wakati wa kuweka shinikizo kwa Israel.

***BBC***

# Afrika kunufaika dola milioni 50 kutoka China

**BEIJING, China**

RAIS wa China Xi Jinping, ametoa ahadi ya zaidi ya dola bilioni 50 kwa ajili ya kufadhili miradi katika mataifa ya Afrika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya China, zaidi ya viongozi 50 wa Afrika na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres wanahudhuria kongamano la wiki moja kati ya China na mataifa ya Afrika.

Akihutubia viongozi hao katika hafla ya ufunguzi wa kongamano hilo mjini Beijing jana, Rais Jinping alisifu uhusiano wa Afrika na China kuwa bora zaidi katika kipindi cha sasa.

Alisema China iko tayari kuimarisha ushirikiano na nchi za Afrika katika sekta ya viwanda, kilimo, miundombinu, biashara na uwekezaji.

„Katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, serikali itakuwa tayari kutoa msaada wa kifedha unaofikia dola bilioni 50.7. Zaidi ya nusu ya kiasi hicho kitakuwa cha mkopo, na kiasi kingine cha dola bilioni 11, kitatolewa katika namna tofauti za misaada ikiwemo dola bilioni 10 kwa mpango wa kuchochea makampuni ya Kichina katika uwekezaji wake." Alisema.

Kiongozi huyo wa China, aliahidi kusaidia katika uundwaji wa nafasi za kazi takribani milioni moja kwa Afrika. Pia msaada wa dola milioni 141 kwa ajili ya kusaidia operesheni za kijeshi barani humo.

Serikali ya China itatoa mafunzo kwa wanajeshi 6,000 na polisi 1,000 na maafisa wa usimamizi wa sheria kutoka Afrika.

Akihutubia pia mkutano huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Guterres, aliwaambia viongozi wa Afrika kwamba kuongezeka kwa uhusiano kati ya China na bara hilo kunaweza kuchochea mapinduzi ya nishati mbadala. China ina rekodi ya kutolewa mifano ya kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kutokomeza umaskini na utaalamu katika fani na stadi mbalimbali.

***DW***

## Tanzania yaomba msaada Wabrazil

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amewaomba wadau wa michezo kutoka Brazil kufungua ofisi nchini ili kutoa huduma ya kimichezo ikiwamo ujuzi, mawazo na kuendeleza vipaji vya wanamichezo wazawa kwa karibu zaidi.

Ndumbaro aliyasema hayo alipokuwa akifanya mazungumzo na wadau hao ambao wako nchini kwa ajili ya kukutana na viongozo wa baadhi ya vyama vya michezo ikiwamo soka na riadha.

"Unajua Brazil wamepiga hatua sana katika michezo kwa hiyo wamekuja kukaa nasi ili tushirikiane nao nasi tupige hatua kama wao, tumekubaliana tudumishe mahusiano katika nchi hizi mbili," Ndumbaro alisema na kuongeza:

"Tumewashauri wafungue ofisi nchini ili waweze kutoa huduma za kimichezo kwa karibu zaidi."

Waziri huyo pia amemshukuru Balozi wa Tanzania nchini Brazil Profesa Adelardus Lubango Kilangi, kwa kazi kubwa aliyofanya ya kuwaleta nchini wadau hao wa maendeleo ya michezo.

Naye Balozi Kilangi ameishukuru serikali kwa mapokezi mazuri na anaimani mazungumzo na wadau hao wa sekta ya michezo kutoka Brazil yatazaa matunda.

## Mlandege: Tunautaka ubingwa wa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MLANDEGE FC imesema ina matumaini itafanya vizuri katika msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar unaotarajiwa kuanza leo kwenye viwanja mbalimbali.

Wakongwe hao wanatarajia kuanza kampeni za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kesho kwa kuwakabili Chipukizi FC kutokea Kisiwani Pemba mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Amaan Complex.

Kocha Mkuu wa Mlandege, Hassan Ramadhani, alisema wamefanya maandalizi ya muda mrefu ili kuhakikisha kikosi chao kinakuwa imara na kucheza soka lenye ushindani.

"Tumefanya maboresho mengi katika kikosi chetu ikiwamo kufanya usajili wa nguvu wa wachezaji ambao watatupa matokeo mazuri msimu huu, tumesajili wachezaji 10 wapya kutoka katika timu za hapa Zanzibar na Tanzania Bara, tunautaka ubingwa," alisema Ramadhani.

Aliongeza anaamini wataanza vyema msimu mpya kwa kuchukua pointi tatu muhimu kwa sababu watakuwa kwenye uwanja wa nyumbani na watahamasishwa na mashabiki wao.

# TABORA UNITED YAJICHIMBIA MAFICHONI IKIWAZA POINTI 9

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Tabora United kimeondoka Tabora Mjini na kwenda kuweka kambi sehemu ambayo haijatajwa kwa ajili ya kujiwinda kuikabili Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Septemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, amesema hawataki timu yao ijulikane ilipoweka kambi kwa sababu wanahitaji kujiimarisha na kuwa imara ili kupata ushindi katika mchezo huo ujao.

Mwagala alisema lengo ni kuwapa benchi la ufundi muda mzuri wa kuandaa kikosi, lakini kuleta utulivu kwa wachezaji wao, kabla ya mechi hiyo dhidi ya Kagera Sugar na nyingine mbili zinazofuata ambazo watacheza nyumbani.

"Tumeamua timu iendelee kukaa kambini, lakini tumeondoka Tabora, tumeweka kambi sehemu ambayo hatusemi, lakini ni nje ya hapa.

Hatutaki kambi yetu ijulikane kwa sababu kocha anahitaji muda zaidi na wachezaji wetu wanahitaji utulivu kwa sababu tunahitaji pointi tisa katika mechi zote tatu tutakazocheza nyumbani, tukianzia na Kagera Sugar," alisema Mwagala.

Aliongeza wanaamini kikosi chao kitaimarisha na kupata pointi tisa kutoka kwenye michezo hiyo mitatu mfululizo ambayo watacheza nyumbani dhidi ya Kagera Sugar, Tanzania Prisons na Fountain Gate.

"Tuna mechi dhidi ya Kagera Sugar, Septemba 11, lakini baada ya hapo tutakuwa na michezo mingine ya nyumbani tukiwaalika Prisons na baadaye Fountain Gate, baada ya hapo tutatoka kwenda Mbeya kucheza dhidi ya KenGold Septemba 28, mwaka huu, sasa kabla hatujaondoka nyumbani mkakati wetu ni kuzipata pointi zote tisa tutakazocheza hapa," Mwagala alisema.

Tabora United imecheza michezo miwili mpaka sasa, ikiwa na pointi tatu, ikichapwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Simba, kabla ya kuifunga Namungo mabao 2-1 na kushika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba yenye pointi sita ndio kinara wa ligi hiyo ikifuatiwa na Singida Black Stars ambayo pia imeshinda mechi zake mbili ilizocheza huku mabingwa watetezi, Yanga wana pointi tatu wakishuka dimbani mara moja na kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.



Wachezaji wa Yanga Princess wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), itakayofanyika kuanzia baadaye mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Dodoma Jiji FC yahamia Babati

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imetangaza itautumia Uwanja wa Tanzanite Kwaraa uliopo Babati, mkoani Manyara katika mechi zake za nyumbani za Ligi Kuu kwa sasa wakati wakiufanyia marekebisho Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji, Moses Mpunga, aliliambia gazeti hili watatumia kama uwanja wake wa nyumbani na wataanza katika mchezo wao dhidi ya Namungo unaotarajiwa kuchezwa Septemba 12, mwaka huu.

Mpunga alisema marekebisho ya uwanja wa Jamhuri yanaendelea vizuri na wanaamini watarejea mapema Dodoma kuendelea na kampeni za kuwania taji hilo la Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunacheza mechi zetu za Ligi Kuu mjini Babati kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa kwa kipindi hiki, na tunaanzia mchezo dhidi ya Namungo, kama marekekebisho yataendelea basi mechi nyingine tunacheza tena hapo, lakini kama utakuwa tayari tutarejea kwenye uwanja wetu," alisema Mpunga.

Bodi ya Ligi imeusimamisha Uwanja wa Jamhuri kutumika katika mchezo wa Ligi Kuu mpaka pale utakapokamilisha vigezo vinavyotakiwa.

Agosti 27, Bodi ya Ligi, ilitoa taarifa hiyo, ikisema kuwa uwanja huo umekosa ubora eneo la kuchezea' ambapo sehemu kubwa ikiwa haina majani ya kutosha na yaliyopo ni dhaifu, jambo linalofanya usiwe salama kwa wachezaji, baada ya hilo ikaitaka Dodoma Jiji itafute uwanja mwingine hadi hapo utakapofanyiwa maboresho.

Dodoma Jiji imecheza mechi mbili mpaka sasa, lakini zote ikipoteza ugenini dhidi ya Mashujaa FC na kulazimishwa suluhu dhidi ya wenyeji Pamba Jiji.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TRIPPIER AGEUKA LULU

KLABU tatu za Uturuki, Fenerbahce, Besiktas na Eyupspor zote zimeonyesha nia ya kumsajili mlinzi wa Newcastle, Kieran Trippier baada ya Saudi Pro League Al-Ittihad pia kujaribu kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 33. ***(Sky Sports)***

### MATIP ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 33, na nyota kutoka Jamhuri ya Ireland, John Egan (31), huku wakitafuta soko la wakala huru kumnunua beki mpya wa kati. ***(Sky Sports)***

### UNITED YAMKAZIA ERIKSEN

MANCHESTER United haiwezi kumruhusu kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 32 kuondoka mwezi huu. ***(Football Insider)***

### ELANGA ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United itajaribu tena kumsajili winga wa Nottingham Forest mwenye umri wa miaka 22 kutoka Sweden, Anthony Elanga, katika dirisha dogo la usajili. (Football Insider)

### SULEMANA NJIA MOJA

AJAX imekubali kwa mkopo mkataba wa mkopo na Southampton kwa mshambuliaji wao mwenye umri wa miaka 22 ambaye ni raia wa Ghana, Kamaldeen Sulemana. ***(Fabrizio Romano)***

### LIVERPOOL, ARSENAL VITANI

LIVERPOOL na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kwa karibu beki wa kati wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 18, Mbrazil Vitor Reis. ***(Caughtoffside)***

### CALVERT-LEWIN HAKIJAELEWEKA

EVERTON ilikataa nafasi ya kumsajili mlinzi wa Chelsea Mfaransa, Axel Disasi, mwenye umri wa miaka 26, na fowadi wa Ivory Coast, David Datro Fofana (21), katika makubaliano ya kubadilishana na straika wa Toffees, Dominic Calvert-Lewin (27). ***(Givemesport)***

### NDALA KUTUA EINDHOVEN

WINGA wa Manchester City, Joel Ndala, mwenye umri wa miaka 18 anafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kujiunga na PSV Eindhoven kwa mkataba wa mkopo ikiwa na masharti ya kununua. ***(Athletic)***

### HAGI AKARIBIA BUCHAREST

MSHAMBULIAJI wa Romania, Ianis Hagi, mwenye umri wa miaka 25 anatazamiwa kukataa nafasi ya kuondoka Rangers na kujiunga na Bucharest FCSB. ***(Football Insider)***

### ARMSTRONG KUTUA VANCOUVER

KIUNGO wa kati wa Scotland, Stuart Armstrong, mwenye umri wa miaka 32, ambaye aliondoka Southampton mwishoni mwa msimu uliopita, anakaribia kuhamia Vancouver Whitecaps. ***(Daily Hive)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, RONALDO NJE BALLON D'OR

Sasa ushindani wabakia kwa Haaland, Vinicius, Mbappe...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo wameachwa katika orodha ya wachezaji wanaowania tuzo ya Ballon d'Or , ikiwa ni mara ya kwanza kwa nyota hao kutoteuliwa tangu mwaka 2003.

Mshindi wa rekodi mara nane Messi, na mpinzani wake wa muda mrefu Ronaldo, ambaye ameshinda Ballon d'Or tano, hawakujumuishwa katika orodha ya wachezaji 30 katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo hiyo itakayotolewa Oktoba 28, mwaka huu.

Vinicius Junior, Rodri, Jude Bellingham, Kylian Mbappé, Erling Haaland na Harry Kane ni miongoni mwa majina yaliyopendekezwa.

Vinicius na Bellingham waliisaidia Real Madrid kushinda LaLiga na taji la 16 la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, huku Haaland ikiongoza Manchester City kubeba taji la Ligi Kuu England.

Mapema msimu huu wa joto, Mbappé hatimaye alijiunga na Madrid baada ya kukaa kwa misimu sita PSG.

Messi, ambaye anajiandaa kurejea kutokana na majeraha akiwa na klabu ya Inter Miami, alishinda tuzo hiyo mwaka jana.

Messi mwenye umri wa miaka 37, alishinda Ballon d'Or yake ya kwanza mwaka 2009, mwanzo wa mfululizo wa miaka minne wa kutwaa tuzo ya kwanza. Aliteuliwa kwa mara ya kwanza mnamo 2006.

Ronaldo na Messi waligeuza shindano hilo kuwa lao wakati wa kilele cha maisha yao- walishinda kwa pamoja mara 13 kutoka 2008.

Uteuzi wa kwanza wa Ronaldo ulikuwa 2004.

Kwa upande wa wanawake, nyota watano wa Marekani wameingia kwenye orodha ya walioteuliwa, akiwamo nahodha na kiungo Lindsey Horan, kipa, Alyssa Naeher na washambuliaji, Trinity Rodman, Sophia Smith na Mallory Swanson, wiki chache baada ya kuwasaidia Wamarekani kushinda medali ya dhahabu ya Olimpiki ya 2024 kwa wanawake kwenye soka.

Aitana Bonmatí, Mariona Caldeney, Patri Guijarro, Salma Paraluelo na Alexia Putellas ndio wachezaji watano wa Hispania walioteuliwa kuwania tuzo hiyo.

Hispania ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye Michezo ya Olimpiki, mwaka mmoja baada ya kushinda Kombe la Dunia.

# HUMMELS ATUA AS ROMA

**ROME,** ITALIA

AS Roma imekamilisha usajili wa beki wa zamani wa Borussia Dortmund, Mats Hummels, kwa uhamisho huru, klabu hiyo ya Serie A imetangaza.

Hummels aliondoka Dortmund baada ya kumalizika kwa mkataba wake msimu huu wa joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 alitumia misimu 13 na timu hiyo ya Bundesliga, na kucheza mechi 508 katika vipindi viwili.

Vyombo vya habari vya Italia viliripoti nyota huyo ametia saini mkataba wa msimu mzima wenye thamani ya Euro milioni 2.5.

Baada ya kuisaidia Dortmund kushinda mataji ya Bundesliga mwaka wa 2010 na 2011, Hummels alisajiliwa na Bayern Munich, ambayo alipitia akademi yake, mwaka wa 2016.

Kufuatia miaka mitatu ya kubeba mataji kwenye Allianz Arena, alirejea Dortmund mwaka wa 2019.

Katika msimu wake wa mwisho huko Dortmund, Hummels alikuwa mchezaji muhimu katika timu hiyo ilipotinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na alianza katika kipigo kutoka kwa Real Madrid kwenye Uwanja wa Wembley.

Hummels ameichezea Ujerumani mechi 78 na alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda Kombe la Dunia 2014 lakini aliachwa nje ya kikosi kwa ajili ya michuano ya Ulaya msimu huu.

Kuwasili kwake Roma kunafuatia kuondoka kwa beki Chris Smalling na kujiunga na Al Fayha inayoshiriki Ligi ya Saudi mapema wiki hii.

Roma wameanza msimu mpya wa Serie A kwa kuchukua pointi mbili pekee katika mechi tatu.




## Olmo: Sijapata shida Barcelona

**BARCELONA,** HISPANIA

DANI Olmo amesema hakupata shida kuzoea maisha Barcelona baada ya kumsajili msimu wa 2024/25 wa LaLiga. Baada ya kucheza jukumu muhimu katika ushindi wa Hispania mwenye Euro 2024 msimu huu wa joto, Olmo kisha akapata uhamisho wa euro milioni 60 kutoka RB Leipzig kurudi Barca, ambako alitoka akiwa mdogo.

Hata hivyo, hali mbaya ya kifedha ya Barcelona ilimaanisha awali hawakumsajili kiungo huyo chini ya kanuni za mshahara wa LaLiga, ingawa jeraha lilimaanisha hakuwa sawa kabisa kuanza kampeni hiyo mpya.

Haikuwa hadi pale mshahara wa Ilkay Gundogan aliyerudi Manchester City ulipoondolewa kwenye vitabu na uthibitisho wa jeraha la muda mrefu la Andreas Christensen ndipo Barca waliweza kumuongeza Olmo kwenye kikosi chao rasmi.

Olmo alicheza mechi yake ya kwanza akitokea benchi katika ushindi wa 2-1 wa Barcelona ugenini dhidi ya Rayo Vallecano, akifunga bao la ushindi dakika za lala salama. Kisha alifunga tena katika mchezo ushindi wa cha 7-0 kutoka kwa Real Valladolid.

Akizungumza na waandishi wa Hispania, Olmo alisisitiza hajavurugwa na sakata hilo ya usajili.

"Binafsi sikuteseka kwa sababu nilijua yatatatuliwa," alisema. „Nilitaka kucheza, lakini ilikuwa ndoto ya kuanza na hiyo ndio nimebaki nayo."

Olmo pia alizungumzia jinsi alivyojifunza Barcelona walikuwa wakipanga kuongeza nia yao kwake wakati wa Euro 2024 na jinsi hatua hiyo ilivyofanikiwa.

"Katika kipindi cha mwisho katika Euro 2024 nilijua kwamba Barcelona walikuwa na nia ya kunisajili," aliendelea.

"Kisha nilikwenda likizo kwa wiki moja, na niliporudi, tulifunga kila kitu. Ilikuwa haraka sana, na wiki mbili baada ya kumalizika kwa michuano ya Ulaya, tulikuwa tumefikia makubaliano.

„Siku zote nimejaribu kujitoa katika timu zote na sasa Barcelona tuna lengo la kushinda. Yeyote anayekuja lazima afanye hivyo kwa mawazo ya ushindi; kama sivyo, ana klabu mbaya. Nataka kushinda na klabu hii na ndiyo maana nipo hapa."



## Diaz asema itakuwa pigo kumkosa Salah

**LIVERPOOL,** ENGLAND

LUIS Diaz amekiri maisha pale Liverpool yatakuwa magumu bila Mohamed Salah ambaye yupo katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake huko Anfield.

Salah alizua wasiwasi baada ya ushindi wa Jumapili wa mabao 3-0 dhidi ya Manchester United, akithibitisha hakuna mtu huko Liverpool aliyeanza majadiliano juu ya mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye alihamia Anfield mwaka 2017, anapaswa kumaliza miaka yake nane huko Merseyside wakati mkataba wake wa sasa unamalizika mnamo Juni mwakani.

Kocha mpya wa Liverpool, Arne Slot alikuwa mwepesi kuzungumza kuhusu uvumi wa kuondoka, akisisitiza kulikuwa na njia ndefu na kuwataka mashabiki kutokuwa na wasiwasi juu ya hatima ya Salah.

Lakini naonekana sio tu mashabiki ambao wana wasiwasi juu ya harakati za Salah, kwa sababu mwenzake Diaz amefunua hisia zake juu ya suala hilo.

"Itakuwa ngumu kwetu," alisema akiiambia Telemundo. „Itakuwa ngumu kwa Liverpool. Itaumiza sana, ana mwaka wa kufikiria juu yake, sio rahisi hata kidogo. Yeye huzungumza nasi kila wakati, itakuwa ngumu sana kupoteza mchezaji kama yeye.

Salah amepata mafanikio makubwa tangu kuhamia Liverpool, kukusanya taji la Ligi Kuu, Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Liverpool imeanza kampeni yao ya 2024/25 na ushindi dhidi ya Ipswich Town, Brentford na Manchester United.

Salah, ambaye amecheza katika kila mchezo, tayari amepachika mabao matatu.



HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS, JKT, YANGA PRINCESS KUWANIA NGAO

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya kuwania Ngao ya Jamii kwa Wanawake yamepangwa kufanyika kuanzia Septemba 24 hadi 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya pili yatashirikisha timu nne zilizomaliza katika nafasi ya juu kwenye msimu uliopita.

Ndimbo alizitaja timu zitakazoshiriki mashindano hayo ni pamoja na mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), Simba Queens, JKT Queens, Yanga Princess zote kutoka Dar es Salaam na Ceasiaa ya mkoani Iringa.

"Tunatarajia kufungua pazia la msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa mashindano ya Ngao ya Jamii, maandalizi yake yanaenda vizuri na michuano hii itaanza kwa kushirikisha klabu nne, tunaamini yatakuwa na ushindani na msisimko mkubwa zaidi ya mwaka jana," Ndimbo alisema.

Naye Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema timu yake iko tayari kwa ajili ya kutetea taji hilo waliloshinda mwaka jana.

Makanya alisema wanaamini watafanya vyema katika mashindano hayo kwa sababu wachezaji wao bado wana ‚joto' la michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), iliyomalizika wiki iliyopita.

"Hakuna mashindano rahisi, tunajua kila timu imejiandaa kufanya vyema, tutakiwa kama washindani, hatutabweteka, tunahitaji kuanza msimu mpya kwa kubeba ngao hiyo," Makanya alisema.

Simba Queens itamkosa kipa wake chaguo la kwanza Mkenya, Caroline Rufa, ambaye aliumia katika michuano ya CECAFA iliyomalizika huko Ethiopia kwa wenyeji CBE kutwaa ubingwa.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu wenye ulemavu wakifanya mazoezi kwenye Uwanja Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Fountain Gate yaitisha KenGold

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, amewaita mashabiki wa soka mkoani Manyara ili kuwashangilia katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KenGold utakaochezwa Septemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa kwa sababu watawapta zawadi ya ushindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Muya, alisema mechi hiyo itakuwa ni siku maalumu kwa mashabiki wao kwa sababu watacheza uwanjani hapo kwa mara ya kwanza na wanataka kuanza na historia nzuri ndani na mkoa huo.

Muya alisema pia wanataka kuweka rekodi ya kushinda mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu mkoani humo.

"Hivi sasa tupo mazoezini, tunajipanga kwa ajili ya mechi ya KenGold, vijana wote wapo imara, itakuwa ni mechi ya kwanza kucheza tukiwa hapa Manyara kwa sababu mechi zetu mbili tulicheza tukiwa nje, itakuwa ni siku maalum kwa mashabiki wa hapa na vitongoji vyake, tunawaomba wajitokeze kwa wingi wa sababu tunataka kuwapa zawadi ya ushindi, ili historia iandikwe kama ya kwanza ligi imechezwa na tumeshinda," alisema Muya.

Fountain Gate iliyoko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi tatu ilianza msimu kwa kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Simba lakini ikapata ushindi magoli 2-0 ugenini dhidi ya Namungo.

## Fadlu aleta mfumo mpya Simba SC

INATOKA UK. 24

kwa ajili ya kupata ushindi katika michezo yao inayokuja.

Alisema ni lazima wawe na njia tofauti ya kupata ushindi na si kutegemea aina moja ya uchezaji.

"Tunataka kuhakikisha michezo yetu ijayo tunapata ushindi, tutaanza na huu wa Kombe la Shirikisho na ile ya Ligi, nataka kuona kikosi kinakuwa imara kwenye idara na kutafuta magoli kwa kila namna," alisema Fadlu.

Katika hatua nyingine, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo amesema kikosi hicho kina wiki nzima sasa kinafanya mazoezi, huku akiweka wazi kuwa wanatarajia kuondoka nchini kati ya Septemba 10-12 kwenda nchini Libya.

"Tutaondoka Septemba kati ya 10, 11, 12 kulingana na upatikanaji wa ndege kwenda kuivaa Al Ahly Tripoli katika mechi yetu ya mkondo wa kwanza wa Kombe la Shirikisho, hatuna sababu ya kwenda mapema kwa sababu tunajua mazingira ya karibu nchi zote za Afrika, tunajua hata hali za hewa za nchi mbalimbali na mazingira yake, kwa hiyo yale mambo ya kwamba lazima tuwahi ili tuzoee mazingira sisi kwetu hayapo tena," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kuwa kikosi hicho kesho kitacheza mchezo mwingine wa kirafiki kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam dhidi ya JKT Tanzania.

"Tutacheza mchezo wetu wa kirafiki Jumamosi Uwanja wa KMC Mwenge, Dar es Salaam dhidi ya JKT Tanzania na ndiyo utakuwa mchezo wetu wa mwisho kabla ya kwenda kuivaa Al Ahly Tripoli.

Mchezo huu wa kirafiki utakuwa na mashabiki, hatuna haja ya kuwakataza mashabiki wetu kuiangalia timu yao, tunawaruhusu waje kwa wingi kuiona Simba yao," alisema Maneja Habari huyo.

Hiyo itakuwa mechi ya pili ya majaribio ya Simba kabla ya kucheza mchezo wao wa kimataifa kwani Jumapili iliyopita ilicheza dhidi ya Al Hilal ya Sudan na kutoka sare ya bao 1-1.

## Wachezaji Stars waapa 'kukiwasha'

INATOKA UK. 24

zaidi kwenye mchezo ujao," alisema Mao.

Kocha wa timu hiyo, Hemed Moroco, alisema Ethiopia ni timu ngumu na walicheza vizuri ndio maana walipata matokeo hayo waliyoyapata.

Alisema licha ya kupambana, walipata upinzani mzuri kutoka kwa wageni wao hao.

Mchezo unaofuata Stars watacheza ugenini, Guinea Septemba 10 huku Ethiopia wakipambana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

# Michezo


Ijumaa Septemba 6, 2024

Nipashe


**Messi, Ronaldo nje Ballon d'Or**

UKURASA 21




Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ,Taifa Stars', Clement Mzize (kulia), akiwatoka mabeki wa Ethiopia kwenye mchezo wa kwanza wa kufuzu fainali za Afrika (AFCON) 2025 juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Timu hizo hazikufungana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Fadlu aleta mfumo mpya Simba SC

## ●●●Awataka wachezaji wake kuushika na kuutumia katika...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids kwa siku za karibuni amekuwa akiwapa wachezaji wake mbinu katika mfumo mpya ambao anataka wawe wanapiga mashuti ya nguvu langoni pale wanapoona ngome ya mpinzani ni ngumu kupitika.

Katika mazoezi ya timu hiyo yanayofanyika kwenye uwanja wa Mo Arena, Bunju, Fadlu ameonekana akiwahimiza wachezaji wake kupiga mashuti kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo na kupunguza aina yao ya uchezaji ya kutaka kuingia mpaka kwenye boksi.

Simba inajiandaa na mechi ya raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli mchezo utakaochezwa ugenini Septemba 15 kwenye Uwanja wa Juni 11, kabla ya marudiano, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Septemba 20 mwaka huu.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini alikuwa akiwatumia wachezaji, Awesu Awesu, Debora Fernandes, Jean Ahoua, Leonel Ateba na Valentino Mashaka kwa ajili ya kupiga mashuti ya mbali.

Mbali na aina hiyo ya mazoezi, kocha huyo pia aliwaelekeza wachezaji wake jinsi gani ya kumalizia mipira ya krosi, ambapo aliwatenga baadhi ya wachezaji kwa ajili ya kupiga mashuti na wengine kumalizia kwa miguu na vichwa.

Katika mazoezi hayo, kiungo Fabrice Ngoma, ambaye amerejea ndani ya kikosi hicho baada ya kutoka kwao, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alipokwenda kwa ajili ya matatizo ya kifamilia, alikuwa akicheza chini kila timu inapoenda kushambulia.

Akizungumza na Nipashe, Fadlu, alisema anaandaa kikosi chake

INAENDELEA UK. 23

# Wachezaji Stars waapa 'kukiwasha' Guinea

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya juzi kushindwa kupata ushindi kwenye mchezo wao wa kwanza wa kufuzu fainali za Afrika (AFCON) 2025 dhidi ya Ethiopia, wachezaji wa timu ya taifa 'Taifa Stars' wameapa kwenda ,kukiwasha' na kupata pointi tatu kwenye mchezo ujao dhidi ya Guinea.

Stars juzi ikiwa nyumbani ilishindwa kupata ushindi kwenye mchezo huo na kulazimishwa kutoka bila kufungana kwenye Uwanja wa Taifa.

Beki wa kati wa timu hiyo, Dickson Job, alisema matokeo waliyoyapata hawakuyakusudia lakini anaamini benchi la ufundi limeona mapungufu yaliyojitokeza na watayafanyia kazi.

"Tulijipanga kupata ushindi, lakini kwa bahati mbaya matokeo ndio hayo, benchi la ufundi litafanyia kazi pale wanapoona hatukufanya vizuri," alisema Job.

Aidha, alisema mchezo ujao ambao watacheza ugenini wataenda kupambana na kuhakikisha wanapata pointi tatu ili kujiweka kwenye mazingira mazuri zaidi.

Beki wa kushoto wa timu hiyo, Mohamed Hussein, alisema matokeo ya juzi hayajawakatisha tamaa na wanakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao.

"Tulitarajia ushindi, lakini mpira una matokeo ya aina tatu, kushinda, kutoka sare au kufungwa, tunaenda kujiandaa kwa mchezo ujao ambapo naamini tutapambana zaidi na kupata ushindi," alisema nahodha huyo wa klabu ya Simba.

Nahodha wa Stars katika mchezo wa juzi, Himid Mao, alisema licha ya pointi moja waliyoipata, matokeo hayo yamewapa hamasa ya kufanya vizuri zaidi kwenye mchezo unaofuata.

"Tulijitahidi kupambana, lakini wapinzani wetu nao walijitahidi kuonyesha uwezo wao, matokeo haya kwetu ni chachu na hamasa ya kupambana

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >